**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU**
MJI WA SERIKALI MTUMBA,
MTAA WA KAZI,
S. L. P. 2890,
DODOMA.

KIMEPIGWACHAPA NA MPIGACHAPA MKUU WA SERIKALI-DODOMA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA WAZIRI MKUU

# KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU

# Mwongozo wa Utekelezaji, Ujumuishwaji na Uimarishaji wa Huduma kwa Watu wenye Ulemavu Tanzania

**OKTOBA, 2022**

# KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU

## Mwongozo wa Utekelezaji, Ujumuishwaji na Uimarishaji wa Huduma kwa Watu wenye Ulemavu Tanzania

# YALIYOMO

YALIYOMO ........................................................ i

**Dibaji**.............................................................................. v

Tafsiri ya Maneno.................................................................. ix

**SURA YA KWANZA** ........................................................ 1

**1.0 UTANGULIZI, MALENGO, WALENGWA NA MPANGILIO WA MWONGOZO**............................ 1

1.1 Utangulizi.......................................................... 1

1.2 Malengo ya Mwongozo........................................... 3

1.3 Walengwa wa Mwongozo......................................... 4

1.4 Mpangilio wa Mwongozo......................................... 5

**SURA YA PILI**.......................................................... 6

**2.0. HALI YA HUDUMA KWA WATU WENYE ULEMAVU**........................................................ 6

2.1. Utoaji wa Huduma kwa Watu wenye Ulemavu Nchini...................................................... 6

2.2. Mafanikio, Upungufu, Fursa na Changamoto.......................................................... 7

**SURA YA TATU**......................................................... 12

**3.0. UTEKELEZAJI, UJUMUISHWAJI NA UIMARISHAJI HUDUMA KWA WATU WENYE ULEMAVU**................................................ 12

3.1. Dira, Dhima na Maadili ya Msingi .......................... 12

3.1.1 Dira............................................................. 12

3.1.2 Dhima.......................................................... 12

3.1.3 Maadili ya Kuzingatiwa na Wadau............................12
3.2 Maeneo Makuu ya Vipaumbele vya Utekelezaji, Ujumuishwaji na Uimarishaji wa Usawa, Haki, Fursa na Huduma kwa Watu wenye Ulemavu ........................................................14
3.2.1 Eneo la Kwanza la Kipaumbele: Utafiti, Takwimu na Ukusanyaji wa taarifa kuhusu Watu wenye Ulemavu.................................................16
3.2.2 Eneo la Pili la Kipaumbele: Ufikivu wa Miundombinu, Usafiri wa Umma, Habari na Mawasiliano kwa Watu wenye Ulemavu ....................17
3.2.3 Eneo la Tatu la Kipaumbele: Afya na Ustawi wa Jamii kwa Watu wenye Ulemavu ............ 21
3.2.4 Eneo la Nne la Kipaumbele: Ubora wa Elimu, Ujuzi, Stadi za Kazi na Stadi za Maisha....................24
3.2.5 Eneo la Tano la Kipaumbele: Ajira, Kazi za Staha, Hifadhi ya Jamii, Uwezeshaji na Ushirikishwaji Kiuchumi kwa Watu wenye Ulemavu ...........................................................27
3.2.6 Eneo la Sita la Kipaumbele: Haki na Ulinzi wa Kisheria.........................................................32
3.2.7 Eneo la Saba la Kipaumbele: Ushiriki na Ushirikishwaji wa Watu wenye Ulemavu katika Nyanja mbalimbali za Kijamii na Kisiasa..............................................................36
**SURA YA NNE.....................................................................40**
**4.0. UTEKELEZAJI WA MWONGOZO NA MAJUKUMU YA WADAU ...................................... 40**
4.1. Mfumo wa Utekelezaji wa Mwongozo.................... 40

4.2. Gharama za Utekelezaji wa Maeneo ya Vipaumbele vya Mwongozo ....................................40
4.3. Matokeo ya Utekelezaji Yanayotarajiwa..... ............40
4.4. Majukumu ya Wadau ...........................................41
4.4.1. Wizara yenye Dhamana ya Masuala ya Watu wenye Ulemavu ...................................................41
4.4.2. Wizara yenye Dhamana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ...............................................42
4.4.3. Mamlaka za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa .........................................................................43
4.4.4. Wizara yenye Dhamana na Masuala ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.............................................44
4.4.5. Wizara zenye Dhamana na Masuala ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum ..................................................44
4.4.6. Wizara zenye Dhamana na Masuala ya Habari, Mawasiliano, Utamaduni, Sanaa na Michezo.........45
4.4.7. Wizara yenye Dhamana na Masuala ya Ujenzi, Miundombinu na Uchukuzi ....................................45
4.4.8. Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali na Taasisi nyingine za Serikali...................45
4.4.9. Sekta Binafsi na Wadau Wengine Muhimu ............46
4.4.10 Shirikisho na Vyama vya Watu wenye Ulemavu.......................................................................47
4.4.11 Watu wenye Ulemavu...............................................48
4.5. Uratibu na Utekelezaji wa Mwongozo.....................48
4.5.1. Serikali…..........................................................................48

4.5.2. Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia ................................49
**SURA YA TANO ........................................................50**
**5.0. UFUATILIAJI, TATHMINI, MAPITIO NA MAREKEBISHO YA MWONGOZO ..........................50**
5.1. Ufuatiliaji na Tathmini ..................................................50
5.2. Mapitio na Marekebisho ya Mwongozo ......................51

## MAELEZO YA WAZIRI MWENYE DHAMANA

Huduma kwa Watu wenye Ulemavu hutolewa kwa ushirikiano wa Wadau mbalimbali, ikiwemo Serikali Kuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wadau wa Maendeleo, Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu, Vyama vya Watu wenye Ulemavu, Asasi zisizo za Kiserikali, Mashirika ya Dini, Watu binafsi na jamii. Huduma hizo hutolewa kwa misingi ya ushirikiano kwa vile Wadau hao pamoja na Serikali wanatambua haki, mahitaji na mchango mkubwa wa Watu wenye Ulemavu katika maendeleo ya jamii na nchi yetu kwa ujumla. Haki, Mahitaji, Mchango na umuhimu wao unaonekana katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii. Mambo haya yameelezwa na kuonekana vema katika matakwa ya Katiba ya Nchi, Sera, Sheria na Miongozo mbalimbali.

Hata hivyo, licha ya kuwepo kwa matakwa hayo ya Kikatiba, Kisera, Kisheria na Miongozo mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa pamoja na juhudi mbalimbali za Serikali na Wadau wengine zinazoendelea kutekelezwa; bado kumekuwa na changamoto kadhaa zinazowakabili Watu wenye Ulemavu, ikiwemo ujumuishwaji hafifu na huduma zisizokidhi hali halisi ya mahitaji yao. Hali hii inatufanya tuhitaji kuwa na mipango imara na miongozo madhubuti itakayotuwezesha kukuza mchango na ushiriki wao katika maendeleo ya Taifa. Hivyo, ni muhimu changamoto zinazowakabili Watu wenye Ulemavu zikafahamika na kutatuliwa kwa njia muafaka ili kuhakikishia kuwa hawaachwi nyuma na kuongeza nafasi ya ujumuishwaji wao katika jamii na maendeleo ya nchi kwa ujumla.

Kwa kulitambua hilo, pamoja na kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 56 ya Kanuni Kuu za Watu wenye Ulemavu za Mwaka 2012, Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano (2021-2026), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha

Mapinduzi katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2025; pamoja na Nyaraka nyinginezo; Serikali imeona ni vema kushirikiana na Wadau na kuandaa Mwongozo huu wa Kitaifa wa Kukuza Ujumuishwaji na Kuimarisha Huduma kwa Watu wenye Ulemavu Tanzania Bara. Mwongozo huu utawasaidia Wadau kwa kuwaonesha Maeneo Makuu ya Vipaumbele watakayoyazingatia katika kuandaa Afua zinazolenga kutatua changamoto kwa Watu wenye Ulemavu. Pia, unasisitiza uwepo wa Afua zinazotambua kwa mapana mahitaji halisi ya Walengwa na kwa mgawanyo sawa unaoendana na mahitaji ya maeneo mbalimbali nchini. Mwongozo huu unatarajiwa vilevile kurahisisha na kuwezesha huduma za uratibu na usimamizi wenye tija na ufanisi wa shughuli na masuala mbalimbali yanayolenga kutatua changamoto za Watu wenye Ulemavu.

Matumaini ya Serikali ni kwamba Wadau wote watazingatia, pamoja na mengineyo, Maadili ya Msingi na Maeneo ya Vipaumbele yanayowekwa na Mwongozo huu katika kuandaa Mipango yao na Afua kwa ajili ya kushughulikia changamoto za Watu wenye Ulemavu. Kwa kutumia Mwongozo huu ni dhahiri kwamba suala la kukuza Ujumuishwaji pamoja na kuimarisha Huduma kwa Watu wenye Ulemavu litakuwa na tija na matokeo makubwa; mazuri na yanayoonekana kiurahisi na kwa haraka katika ngazi na nyanja zote za maisha ya jamii yetu. Vilevile, Mwongozo utarahisisha Ufuatiliaji na Tathmini na hivyo kutuwezesha kufahamu maeneo yanayohitaji muitikio wa haraka.

Kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, natoa wito kwa Wananchi na Wadau Wote wa Sekta ya Umma na Binafsi Tanzania Bara, kushiriki kikamilifu na kujitolea kwa hali na mali; na kutenga angalau sehemu ya rasilimali walizonazo, kama wajibu wao wa lazima waliojiwekea wenyewe kwa hiari katika kuhudumia, kuonesha

na kurudisha hisani kwa jamii; ili kuhakikisha kuwa malengo ya kukuza ujumuishwaji na kuimarisha huduma kwa Watu wenye Ulemavu yanafikiwa kikamilifu na wao kuwa sehemu ya mafanikio hayo.

Aidha, tunatambua na kuthamini ushirikiano mkubwa na umuhimu uliopo baina ya Serikali na Wadau wengine katika uandaaji wa Mwongozo huu. Uandaaji na ukamilishwaji wa Mwongozo umewezekana kutokana na michango ya hali na mali kutoka kwa Wadau; ikiwemo maoni na ushauri walioutoa juu ya Maeneo Makuu ya Vipaumbele na masuala muhimu yanayopaswa kuwemo ndani ya Mwongozo. Inaweza isitoshe kuwatambua na kuwashukuru kwa kuwataja mmoja mmoja hapa; lakini ni vema nitumie fursa hii kuwashukuru wote walioshiriki kwa namna moja ama nyingine katika kufanikisha maandalizi na ukamilishwaji wa Mwongozo. Siyo vibaya pia nikiwashukuru kwa kuwataja wachache ambao wamewezesha kufanikiwa kwa zoezi la uandaaji na ukamilishaji wa Mwongozo.

Kwanza kabisa ninawashukuru Viongozi, Watendaji na Watumishi wote wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu walioshiriki kuanzisha na kuratibu uandaaji na ukamilishwaji wa Mwongozo. Utaalamu na uvumilivu wao umekuwa nyenzo na mahali muhimu pa kuanzia katika kufanikisha uwepo wa Mwongozo huu muhimu kwa ajili ya Kukuza Ujumuishwaji na Kuimarisha Huduma kwa Watu wenye Ulemavu nchini. Wadau wengine wa Serikali ni pamoja na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Afya, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Baraza la Ushauri la Taifa kwa Watu wenye Ulemavu na wengineo ambao sijaweza kuwataja hapa.

Shukurani za kipekee ziende kwa Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA) na Vyama vilivyo chini yake; ambao wameshiriki kwa hali na mali katika hatua mbalimbali za uandaaji na ukamilishwaji wa Mwongozo huu. Vilevile, ninawashukuru Wadau wengine wote waliojitokeza na kutoa michango yao ya hali na mali wakati wa uandaaji wa Mwongozo huu, yakiwemo Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa na Asasi za Kijamii. Miongoni mwao wapo Foundation for Civil Society, ADD International, CBM International, Sight Savers, Standing Voice, Light for the World, Haki Elimu na PACT TANZANIA. Michango yao ndiyo iliyowezesha uandaaji wa Mwongozo wenye mtizamo wa kuwaleta kwa pamoja Wadau wa Sekta ya Umma na Binafsi ili kutatua changamoto walizonazo Watu wenye Ulemavu nchini.

Mwisho, napenda kusisitiza kuwa suala la Kukuza Ujumuishwaji na Kuimarisha Huduma kwa Watu wenye Ulemavu ni la jamii nzima. Hivyo, Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu tunatambua, tunaheshimu na kuzingatia wakati wote kwamba, kila Mdau ana mchango muhimu katika suala zima la ujumuishaji na uimarishaji wa utoaji na upatikanaji wa huduma bora kwa Watu wenye Ulemavu nchini.

Hivyo, tutekeleze kikamilifu Mwongozo huu wa Kukuza Ujumuishwaji na Kuimarisha Huduma kwa Watu wenye Ulemavu Tanzania, kwa pamoja na mingine iliyopo, kwa ajili ya Maendeleo na Ustawi wa Watu wenye Ulemavu na Taifa letu kwa ujumla.

**MHE. PROF. JOYCE L. NDALICHAKO (Mb.)**
*Waziri wa Nchi - Ofisi ya Waziri Mkuu*
*(Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu)*

## Dibaji

Tanzania ni nchi yenye demokrasia imara inayojengwa kwa kufuata misingi thabiti ya kuheshimu, kutambua na kuthamini utu, usawa na haki kwa watu wote bila ya ubaguzi wa aina yoyote. Kila mtu na kila mwananchi wakiwemo Watu wenye Ulemavu, wana haki sawa ya Kikatiba na Kisheria ya kushiriki kikamilifu katika mambo muhimu yanayomhusu yeye mwenyewe na jamii nzima kwa ujumla, ikiwemo kupata mahitaji ya msingi. Hivyo, upo umuhimu wa kutambua uwezo na mchango wa Watu wenye Ulemavu mahali popote walipo na kuweka mikakati thabiti ya kuwaendeleza na kuwahakikishia ustawi na mahitaji yao ya kimsingi, ikiwemo ulinzi na usalama wao. Hii ni pamoja na kujumuishwa katika Nyanja zote za kijamii, kisiasa na kiuchumi ili kuinua ustawi na maisha yao; na kuwafanya wawe na mchango zaidi katika maendeleo ya jamii zao na Taifa kwa ujumla.

Kwa kutambua hayo, hatua mbalimbali zimekuwa zikichukuliwa katika ngazi ya Kitaifa na Kimataifa; ikiwemo kuweka na kutekeleza Mikataba, Itifaki, Mipango na Mikakati anuwai ya muda mrefu na mfupi; ya kuwahakikishia Watu wenye Ulemavu ustawi na maisha jumuishi yenye staha na kuthamini utu wao.

Hata hivyo, hali ya huduma na ustawi kwa Watu wenye Ulemavu nchini na duniani kote, bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zinahitaji kuendelea kuwekewa mipango na mikakati mahususi ya kuzipatia ufumbuzi kwa kuzingatia mahitaji halisi ya walengwa. Tanzania, bado inahitaji kuendelea kukuza ujumuishwaji na kuimarisha utoaji na upatikanaji wa huduma kwa Watu wenye Ulemavu; na hapa ndipo unapokuja umuhimu wa kuwa na Mwongozo wa Utekelezaji, Ujumuishwaji na Uimarishaji wa Huduma kwa Watu wenye Ulemavu Tanzania.

Hivyo, madhumuni na maudhui ya Mwongozo huu kama ilivyo kwa nyaraka nyinginezo, pamoja na hatua mbalimbali zilizokwishachukuliwa na Serikali na Wadau katika ngazi ya Kitaifa na Kimataifa; ni kutoa mwelekeo, miongozo na maelekezo kwa Viongozi na Watendaji wa Serikali pamoja na Wadau wengine katika ngazi mbalimbali, ili kuchochea maendeleo na ustawi wa Watu wenye Ulemavu kwa kuongeza hatua za ujumuishwaji na kutoa huduma bora kwao ili kuwawezesha kukabiliana na changamoto za kimaisha zitokanazo na zinazochochewa na hali ya ulemavu walionao. Pia, Mwongozo umelenga kurekebisha Sera, Mitizamo, Mienendo na Vitendo vyote visivyolinda na vinavyonyima haki na nafasi kwa Watu wenye Ulemavu kushiriki kwenye maamuzi na utekelezaji wa masuala muhimu ya kijamii, kisiasa na kiuchumi.

Mwongozo huu unakusudiwa kuwa wa muda mrefu unaoweka na kutoa Dira na Mwelekeo wa Vipaumbele muhimu vya Kitaifa katika Ujumuishwaji, Utoaji na Upatikanaji wa Huduma Bora kwa Watu wenye Ulemavu nchini.

Kama nchi tunahitaji kuwa na jamii jumuishi inayozingatia Haki, Usalama, Usawa na Huduma Bora kwa Watu wenye Ulemavu. Hii itafikiwa kwa kuhakikisha uwepo wa Ujumuishwaji, Uimarishaji na Upatikanaji wa Huduma Bora kwa Watu wenye Ulemavu nchini unaotokana na kuimarishwa kwa Sera, Sheria, Miongozo na Mifumo mbalimbali ya Uratibu, Usimamizi, Utekelezaji, Ufuatiliaji na Tathmini kwa Ushirikiano wa wadau.

Haya yote yatafikiwa iwapo Wadau watazingatia Maadili ya kimsingi yakiwemo ya Uwajibikaji, Utii, Uwazi, Ushirikiano, Ushirikishwaji na kuthamini na kutambua Utu wa kila Mtu.

Mwongozo huu unabainisha Maeneo Makuu Saba ya Kipaumbele ya kujielekeza kimkakati ambayo ni Utafiti na upatikanaji wa Taarifa na Takwimu kuhusu Watu wenye Ulemavu; Ufikivu wa Miundombinu, Usafiri wa Umma, Habari na Mawasiliano kwa Watu wenye Ulemavu; Afya na Ustawi kwa Watu wenye Ulemavu; Elimu, Ujuzi na Mafunzo ya Stadi za Kazi; Upatikanaji wa Ajira, Kazi za Staha, Kinga na Hifadhi ya Jamii, Uwezeshaji na Ushirikishwaji Kiuchumi kwa Watu wenye Ulemavu; Haki na Ulinzi wa Kisheria kwa Watu wenye Ulemavu; na Ushiriki na Ushirikishwaji wa Watu wenye Ulemavu katika nyanja mbalimbali za Kijamii na Kisiasa.

Maeneo hayo Saba ya Vipaumbele vya Kimkakati ndiyo yanayopaswa kuzingatiwa na Wadau wote wa Sekta ya Umma na Binafsi wakati wa kuandaa Mipango na Bajeti zao; pamoja na hatua zote za utekelezaji wa majukumu yao, mijini na vijijini nchini kote.

Hivyo, Wadau wa Huduma kwa Watu wenye Ulemavu katika ngazi zote nchini, wana fursa na wanapaswa kuandaa mipango mikakati, mipango kazi ya utekelezaji wa shughuli stahiki ya muda mrefu, kati na mfupi pamoja na bajeti zitakazowawezesha kutekeleza shughuli zao kila mwaka, kwa kuzingatia mwelekeo unaoelezwa ndani ya Mwongozo. Wadau hawa wana hiari ya kuchagua maeneo mahususi ya kujielekeza miongoni mwa Vipaumbele Saba vilivyobainishwa ndani ya Mwongozo kulingana na malengo na maudhui ya shughuli zao. Hatua hii itasaidia pia kuleta wepesi katika suala zima la Usajili, Uratibu, Usimamizi, Tathmini na Ufuatiliaji wa Miradi na Shughuli za Asasi na Taasisi zinazokusudia kutoa huduma na kufanya kazi kwa ajili ya Watu wenye Ulemavu nchini. Ushiriki wa Wizara, Idara, Taasisi za Serikali, Taasisi Binafsi na Mashirika ya Umma

utakuwa umerahisisishwa, kuhuishwa, kusimamiwa na kuratibiwa ipasavyo.

Kufanikiwa kwa Mwongozo huu kutategemea kuwepo na kuendelea kuimarishwa kwa ushiriki, ushirikiano, ushirikishwaji na mashauriano baina ya Wadau wote wa Kukuza Ujumuishwaji na Kuimarisha Huduma kwa Watu wenye Ulemavu nchini. Matarajio ni kwamba mambo yote yaliyoelezwa na kuelekezwa katika Mwongozo yakizingatiwa na kutekelezwa ipasavyo, nchi yetu itaweza kufikia Dira ya kuwa na “Jamii inayoongoza katika kuzingatia Haki, Usalama, Usawa na Huduma Bora na Jumuishi kwa Watu wenye Ulemavu.”



**PROF. JAMAL ADAM KATUNDU**
*Katibu Mkuu*
*Ofisi ya Waziri Mkuu*
*(Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu)*

## TAFSIRI YA MANENO

**Afua:** Ni shughuli au kazi mbalimbali zilizobainishwa katika Mwongozo.

**Huduma za utengemao;** Humaanisha huduma zinazomwezesha mtu mwenye matatizo ya kijamii, kumudu maisha yake ya kila siku na pia kushiriki kikamilifu katika kuiletea maendeleo jamii inayomzunguka.

**"Lugha"-** Ni neno linalojumuisha lugha ya mazungumzo na lugha ya alama, Lugha ya Mguso na aina nyingine za lugha zisizo za matamshi.

**"Mamlaka za Serikali za Mitaa":** Inajumuisha Mamlaka za Serikali katika ngazi za Vitongoji, Vijiji/Mitaa, Kata, Mji Mdogo, Halmashauri, Miji, Manispaa na Majiji.

**"Mawasiliano" -** Ni neno lenye kujumuisha lugha mbalimbali, maonesho ya matini, maandishi ya "braille", lugha ya kupapasa, maandishi yaliyokuzwa, vyombo mbalimbali vya habari vinavyopatikana, hali kadhalika na maandishi, sauti, lugha nyepesi, ving'amuzi vya vitendo, teknolojia za kukuza mawimbi ya sauti na namna, njia na mitindo mbadala ya kimawasiliano kulingana na aina mbalimbali za ulemavu, ikijumuisha upatikanaji wa taarifa na teknolojia ya mawasiliano.

**"Marekebisho stahili" -** Ni neno linalomaanisha mabadiliko na marekebisho ya lazima na yanayofaa bila kusababisha taabu isiyowiana au isiyovumilika, pale yanapohitajika kutokana na hali fulani, ili kuhakikisha kuwa Watu wenye Ulemavu wanafurahia au kutumia haki zote za binadamu na uhuru wa msingi kwa kiwango sawa na wengine.

**“Ubaguzi kwa misingi ya ulemavu” -** Ni neno linalomaanisha kutofautishwa kokote, kutengwa au kuzuiwa kwa sababu ya ulemavu kwa azma ya kudhoofisha au kubatilisha utambulisho, ufurahiaji au utekelezwaji wa haki zote za kibinadamu na uhuru wa asili kisiasa, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, kiraia au eneo lolote lile kwa misingi ya usawa na watu wengine. Ubaguzi ni pamoja na aina zote za ubaguzi, ikijumuisha na kunyimwa marekebisho stahili.

**“Usanifu kwa ajili ya wote” -** Ni neno linalomaanisha ubunifu wa bidhaa, mazingira, mwongozo na utoaji huduma unaoweza kutumiwa na watu wote, kwa kiasi kikubwa kadri inavyowezekana, bila ya kuwepo haja ya kufanya marekebisho au matengenezo maalum. “Usanifu kwa ajili ya wote” hauondoi umuhimu wa kuwepo kwa nyenzo saidizi kwa ajili ya Watu wenye Ulemavu pale ambapo zinahitajika.

**“Wadau”** Watu au Taasisi katika Sekta ya Umma na Binafsi wanaojishughulisha na masuala ya Watu wenye Ulemavu na wanaoguswa kushiriki katika masuala ya Watu wenye Ulemavu.

**Wadau wa Maendeleo:** Ni Taasisi/Mashirika au watu binafsi wanaoshiriki katika utekekezaji wa miradi na programu za Serikali za maendeleo. Hii inahusisha Mashirika ya Kimataifa, Asasi za Kiraia, Mashirika ya Dini, Sekta Binafsi na Jamii.

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI, MALENGO, WALENGWA NA MPANGILIO WA MWONGOZO

### 1.1 Utangulizi

Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025, Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2004, Sheria ya Watu wenye Ulemavu, Na. 9 ya mwaka 2010, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi. Mpango wa Taifa wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/2022-2025/2026); Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu wa Mwaka 2006, Mkataba wa Marrakesh wa mwaka 2013, Dira ya Jumuiya ya Afrika Mashariki 2050; Dira ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika 2050; Ajenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Dunia, 2030, zinasisitiza umuhimu wa kuchochea maendeleo; kutoa huduma bora; na kutoa nafasi kwa watu wakiwemo wenye Ulemavu kushiriki katika maamuzi na utekelezaji wa masuala muhimu yanayowahusu katika jamii.

Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na wenye Ulemavu ambayo ndiyo yenye dhamana na masuala ya Watu wenye Ulemavu ikiwemo la upatikanaji takwimu na taarifa mbalimbali za Watu wenye Ulemavu. Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 Watu wenye Ulemavu walikuwa milioni 3.4, sawa na asilimia 9.3 ya watanzania wote. Kulingana na Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 idadi ya Watu ni 61,741,120 hivyo inatarajiwa pia idadi ya Watu wenye Ulemavu kuongezeka ikizingatiwa ushirikishwaji wa Watu wenye Ulemavu ulikuwa mkubwa na hivyo kuongeza hamasa ya kushiriki. Pia, inao wajibu wa kuhakikisha

matakwa mbalimbali yaliyomo katika miongozo hiyo yanatekelezwa na imeona ni wakati muafaka kushirikiana na Wadau wengine kutoa Mwongozo utakaosaidia kukuza ujumuishwaji na kuimarisha huduma kwa Watu wenye Ulemavu; na kuhakikisha kwamba changamoto zote zinafanyiwa kazi na kupatiwa ufumbuzi kwa kuzingatia mahitaji na ustawi wao. Vilevile, Mwongozo umekusudiwa kuhakikisha kuwa kila Mdau anashirikishwa na kushiriki kikamilifu na kwa ufanisi katika suala zima la kukuza ujumuishwaji na kutoa huduma bora kwa Watu wenye Ulemavu, kwa usawa na haki.

Serikali, kwa kushirikiana na Wadau; na kwa kutambua na kuthamini mchango mkubwa ambao umekuwa ukiendelea kutolewa na Wadau hao katika kuhudumia Watu wenye Ulemavu nchini; imeona umuhimu wa kuandaa Mwongozo wa Kitaifa unaoelekeza Wadau mbalimbali katika kukuza ujumuishwaji na kuimarisha huduma zao na kuwawezesha kuandaa Afua zinazolenga kuwa na matokeo makubwa zaidi, yanayopimika na kuonekana kirahisi katika kutatua changamoto za Watu wenye Ulemavu nchini. Mwongozo unasisitiza kuimarisha utekelezaji wa Afua na shughuli za Wadau zinazotambua na kuzingatia kwa kina suala la kukuza ujumuishwaji, usawa na haki kulingana na mahitaji halisi ya Watu wenye Ulemavu waliopo katika maeneo mbalimbali nchini, kwa mgawanyo wenye uwiano sawa. Vilevile, Mwongozo unatarajiwa kuwezesha na kurahisisha majukumu ya uratibu, usimamizi, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ili kuyafanya yawe yenye tija na ufanisi katika kutatua changamoto za Watu wenye Ulemavu.

**Mwongozo wa Utekelezaji, Ujumuishwaji na Uimarishaji wa Huduma kwa Watu wenye Ulemavu Tanzania** unabainisha **Maeneo Makuu ya Vipaumbele** yenye kutoa maelekezo na mwelekeo kwa shughuli za wadau zinazolenga

kuimarisha utekelezaji, ujumuishaji, upatikanaji na utoaji wa Huduma Bora kwa Watu wenye Ulemavu nchini. Mwongozo unawahakikishia Watu wenye Ulemavu ujumuishwaji, ulinzi, usalama, haki, kuthaminiwa na kupatiwa huduma stahiki na wezeshi ili kujitegemea na kunufaika kiuchumi, kisiasa na kijamii na kuchangia katika maendeleo ya jamii na taifa kwa ujumla; kama inavyoelekezwa na matakwa ya Kanuni ya 56 ya Kanuni Kuu za Watu wenye Ulemavu za Mwaka 2012, zilizotolewa kupitia Tangazo la Serikali, Namba 152 chini ya Kifungu cha 61 cha Sheria ya Watu wenye Ulemavu, Namba 9 ya Mwaka 2010 zikisomwa kwa pamoja na Mipango, Mikakati, Sera na Itifaki za Kitaifa na Kimataifa, kama ilivyoelezwa hapo awali. Wadau wote wana uhuru na haki ya kuchagua Maeneo ya Vipaumbele vya Mwongozo wanayohitaji kujielekeza kiutekelezaji bila ya kuathiri malengo na maudhui ya shughuli zao, ili mradi watazingatia, muda wote, maadili ya msingi yaliyowekwa na kukubalika na Wadau kupitia Mwongozo.

## 1.2 Malengo ya Mwongozo

### 1.2.1. Lengo Kuu

Lengo Kuu la Mwongozo ni kuelekeza kuhusu Utekelezaji, Ujumuishwaji na Uimarishaji wa Usawa, Haki, Fursa na Huduma kwa Watu wenye Ulemavu.

### 1.2.2. Malengo Mahususi

(a) Kutoa mwongozo katika kuandaa Afua zinazolenga kutatua changamoto za Watu wenye Ulemavu;

(b) Kuainisha maeneo ya kipaumbele yanayopaswa kutekelezwa na kuhakikisha kunakuwepo ujumuishwaji ulio timilifu;

(c) Kuainisha hatua mahususi zinazopaswa kuchukuliwa katika kuhakikisha huduma bora zinapatikana na kutolewa kwa Watu wenye Ulemavu;

(d) Kuainisha Afua zinazotambua kwa mapana na kwa mgawanyo sawa unaoendana na mahitaji halisi ya maeneo mbalimbali nchini;

(e) Kuweka uratibu, usimamizi na utekelezaji wenye tija na ufanisi wa shughuli na masuala mbalimbali yanayolenga kutatua changamoto za Watu wenye Ulemavu;

(f) Kutoa tafsiri ya ujumuishwaji na huduma bora; na umuhimu wake katika jamii ili kuimarisha utekelezaji wa masuala ya Watu wenye Ulemavu; na

(g) Kuwezesha uwepo wa Mipango Shirikishi na Jumuishi ya huduma kwa Watu wenye Ulemavu kwenye maeneo yote ya umma na binafsi, ili kuleta tija na ufanisi katika upatikanaji na utoaji huduma hapa nchini.

## 1.3 Walengwa wa Mwongozo

Walengwa wa Mwongozo ni Wizara, Idara, Taasisi na Wakala za Serikali, Mashirika ya Umma, Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika ya Kimataifa na Kitaifa, Wadau wa Maendeleo, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Asasi za kiraia, Vyama vya Watu wenye Ulemavu, Sekta Binafsi, Taasisi za Dini, Watu wenye Ulemavu waliopo sehemu mbalimbali Tanzania Bara na jamii kwa ujumla ambao ndio Wadau wa usimamizi, uratibu na utekelezaji.

## 1.4 Mpangilio wa Mwongozo

Mwongozo umegawanyika katika sura kuu tano. Sura ya Kwanza ni Utangulizi, Malengo, Walengwa na Mpangilio wa Mwongozo; Sura ya Pili inahusu Hali ya Huduma kwa Watu wenye Ulemavu; Sura ya Tatu inaainisha Dira, Dhima na hatua mahususi za kuchukuliwa katika Maeneo ya Kipaumbele ili kufikia malengo ya Mwongozo ya Utekelezaji, Ujumuishwaji na Uimarishaji wa Huduma kwa Watu wenye Ulemavu nchini. Sura ya nne inaainisha utaratibu wa Utekelezaji wa Mwongozo na Majukumu ya Wadau; na Sura ya tano inaainisha Ufuatiliaji, Tathmini, Mapitio na Marekebisho ya Mwongozo.

# SURA YA PILI

## 2.0. HALI YA HUDUMA KWA WATU WENYE ULEMAVU

### 2.1. Utoaji wa Huduma kwa Watu wenye Ulemavu Nchini

Huduma kwa Watu wenye Ulemavu hapa nchini zimeendelea kutolewa kwa kuzingatia maelekezo yaliyomo katika Nyaraka na Miongozo mbalimbali ilivyoainishwa katika aya ya kwanza ya utangulizi.

Pamoja na mengineyo, malengo, maudhui na mawanda ya Nyaraka na Miongozo tajwa hapo juu ni kuelekeza kwa Serikali na Wadau wengine katika ngazi mbalimbali ili kuchochea maendeleo na ustawi wa Watu wenye Ulemavu kwa kutoa huduma bora kwao na kuwawezesha kumudu makali na changamoto za kimaisha zitokanazo na hali ya ulemavu walionao. Pia, Nyaraka na Miongozo hii imelenga kurekebisha Sera, Mitizamo, Mienendo na Vitendo vyote visivyolinda na visivyotoa haki kwa Watu wenye Ulemavu, pamoja na vile vinavyowanyima nafasi ya kushiriki katika maamuzi na utekelezaji wa masuala muhimu katika nyanja mbalimbali za kijamii, kiuchumi na kisiasa.

Hata hivyo, licha ya uwepo wa huduma hizo na utekelezaji wa Nyaraka na Miongozo hiyo kwa muda mrefu; hali ya huduma na ustawi kwa Watu wenye Ulemavu nchini, pamoja na uwepo wa mafanikio mbalimbali bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zinahitaji kuendelea kuwekewa Mipango na Mikakati mahususi; mara kwa mara, ili kuzitatua kwa kuzingatia mahitaji ya wakati, eneo na kundi husika. Nchini Tanzania, bado kuna uhitaji wa kuendelea kuongeza uelewa wa dhana yenyewe ya ulemavu; kuondoa unyanyapaa, dhana na imani potofu miongoni mwa wanajamii

kwa ujumla, ikiwemo Watu wenye Ulemavu wenyewe; kukuza ujumuishwaji, kuimarisha ufikivu wa miundombinu, uwezeshwaji, ushikikishwaji na upatikanaji wa huduma bora kwa Watu wenye Ulemavu kwa kuhakikisha kunakuwa na upangaji, utekelezaji, uratibu na usimamizi thabiti wa yale yote yanayoelezwa katika Miongozo ya Kitaifa na Kimataifa; ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini stahiki ya maendeleo ya utekelezaji na ujumuishwaji wa masuala ya Watu wenye Ulemavu katika sekta mbalimbali nchini.

Kwa msingi huo, Serikali imeandaa Mwongozo huu ili kuinua kiwango cha utekelezaji, ujumuishwaji, uimarishaji wa huduma na uratibu unaofanywa na mamlaka mbalimbali kwa kushirikiana na wadau wanaoshughulika na masuala ya Watu wenye Ulemavu na hatimaye kuwa na jamii jumuishi inayoongoza katika kutoa huduma bora kwa Watu wenye Ulemavu.

## 2.2. Mafanikio, Upungufu, Fursa na Changamoto

Mwongozo umeainisha mafanikio, mapungufu, fursa na changamoto kuhusu hali ya ujumuishwaji wa huduma kwa Watu wenye Ulemavu Tanzania Bara umezingatia maoni na mapendekezo yaliyotokana na majadiliano na mashauriano na Wadau wanaohusika na utoaji na upatikanaji wa Huduma kwa Watu wenye Ulemavu. Aidha, uchambuzi huu umehusisha pia mapitio ya nyaraka mbalimbali kama zilivyoainishwa hapo awali. Mafanikio, mapungufu, fursa na changamoto za utoaji wa huduma kwa Watu wenye Ulemavu zinaainishwa hapa chini;

### 2.2.1. Mafanikio Yaliyopo

(a) Uwepo wa Sera, Sheria, Mipango na Mikakati mbalimbali ya ujumuishwaji na kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora kwa Watu wenye Ulemavu;

(b) Uwepo Taasisi za kiserikali na zisizo za kiserikali ambazo zinajishughulisha na utoaji wa huduma mbalimbali kwa Watu wenye Ulemavu;

(c) Kuongezeka kwa kampeni kuhusu utetezi na ushawishi wa kupinga unyanyapaa na ukatili dhidi ya Watu wenye Ulemavu;

(d) Uanzishwaji na uendeshaji wa madawati katika ngazi za Wizara, Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma na Binafsi kwa ajili ya kuratibu na kusimamia uimarishaji huduma na ujumuishwaji wa masuala ya Watu wenye Ulemavu.

(e) Uanzishwaji na uendeshaji wa Baraza la Ushauri la Taifa la Watu wenye Ulemavu;

(f) Serikali kuendelea kutoa huduma na kugharamia mahitaji ya Watu wenye Ulemavu katika Sekta mbalimbali ikiwemo Elimu na Afya;

(g) Uwepo na utekelezwaji wa programu mbalimbali za Serikali na Wadau za uwezeshaji kiuchumi kwa Watu wenye Ulemavu;

(h) Kufanyika kwa tafiti kuhusu haki na ustawi kwa Watu wenye Ulemavu hapa nchini;

(i) Kuendelea kuelimisha na kuhamasisha kuhusu haki na ustawi kupitia maadhimisho ya Kimataifa na Kitaifa ya Watu wenye Ulemavu kila mwaka;

(j) Uwepo wa Vyuo na Vituo Maalumu vya utoaji wa huduma ya mafunzo ya stadi za kazi na huduma za marekebisho kwa Watu wenye Ulemavu nchini; na

(k) Uanzishwaji na uendeshaji wa Kamati za Watu wenye Ulemavu katika ngazi ya Mikoa, Halmashauri, Vijiji na Mitaa nchini kote.

### 2.2.2. Upungufu

(a) Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2004 kutofanyiwa mapitio kwa muda mrefu;

(b) Uwepo wa baadhi ya Sera, Sheria na Miongozo inayokinzana katika kuhudumia Watu wenye Ulemavu;

(c) Uwepo wa vikwazo vya ufikivu wa kimazingira, taarifa na vyombo vya usafiri ikiwemo miundombinu isiyo rafiki na vifaa visivyokidhi mahitaji ya Watu wenye Ulemavu;

(d) Upungufu katika uratibu, udhibiti na upatikanaji wa vifaa saidizi kwa Watu wenye Ulemavu;

(e) Upungufu wa wataalamu wa viungo na mazoezi kwa ajili ya huduma za kiafya;

(f) Upungufu wa wataalamu na walimu wa kufundisha elimu maalumu;

(g) Upungufu wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia kwa ajili ya Watoto wenye Ulemavu;

(h) Upungufu wa huduma za ulinzi na usalama kwa Watu wenye Ulemavu katika jamii;

(i) Upungufu wa Watumishi katika Taasisi za Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi kwa Watu wenye Ulemavu; na

(j) Upungufu katika mfumo wa uratibu, usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za wadau wa utoaji huduma kwa Watu wenye Ulemavu nchini.

### 2.2.3. Fursa

(a) Uwepo wa Wadau wengi walio tayari kusaidia masuala ya Watu wenye Ulemavu;

(b) Uwepo wa programu mbalimbali za uwezeshaji kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa Watu wenye Ulemavu;

(c) Uwepo wa mifumo inayoweza kusaidia utekelezaji, uratibu, usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya utoaji wa huduma kwa Watu wenye Ulemavu, katika ngazi zote nchini;

(d) Utayari wa Serikali katika kukuza ujumuishwaji na kuimarisha huduma kwa Watu wenye Ulemavu; na

(e) Uwepo wa Wizara inayoshughulikia masuala ya Huduma kwa Watu wenye Ulemavu.

### 2.2.4. Changamoto

(a) Uelewa mdogo na uzingatiaji hafifu wa jamii juu ya Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali unaodhoofisha usimamizi, uratibu na utekelezaji wake;

(b) Mwamko na utashi duni juu ya ulinzi, usalama, haki na huduma kwa Watu wenye Ulemavu miongoni mwa wanajamii na wadau;

(c) Mitizamo hasi, mila na desturi potofu miongoni mwa wanajamii, wakiwemo Watu wenye Ulemavu wenyewe kuhusu dhana nzima ya ulemavu;

(d) Kutokuwepo kwa rasilimali watu na fedha inayokidhi mahitaji ya Watu wenye Ulemavu;

(e) Umasikini miongoni mwa Watu wenye Ulemavu na familia zao;

(f) Upatikanaji usio wa uhakika wa taarifa na takwimu sahihi za Watu wenye Ulemavu;

(g) Kuwepo kwa Mazingira na miundombinu isiyo rafiki kwa Watu wenye Ulemavu kupata fursa mbalimbali za kisiasa, kiuchumi na kijamii;

(h) Ushiriki na Ushirikishwaji hafifu wa Watu wenye Ulemavu kwenye masuala ya kiuchumi, kijamii na kisiasa.

## SURA YA TATU

## 3.0. UTEKELEZAJI, UJUMUISHWAJI NA UIMARISHAJI HUDUMA KWA WATU WENYE ULEMAVU

### 3.1. Dira, Dhima na Maadili ya Msingi

#### 3.1.1. Dira

Kuwa na Jamii inayozingatia haki, usalama, usawa, huduma bora na jumuishi kwa Watu wenye Ulemavu.

#### 3.1.2. Dhima

Kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora na jumuishi kwa Watu wenye Ulemavu kwa kuimarisha usimamizi na utekelezaji wa Sera, Sheria, Miongozo na Mifumo mbalimbali ya uratibu, ufuatiliaji na tathmini.

#### 3.1.3. Maadili ya Kuzingatiwa na Wadau

Ili kufanikisha kuwepo kwa huduma bora na jumuishi kwa Watu wenye Ulemavu nchini, Wadau wote wanaotoa na wanaopokea huduma hizo wanapaswa kuzingatia "Maadili ya Msingi" yafuatayo:

**(a) Uwajibikaji**

Kila Mdau anapaswa kuweka kipaumbele katika uwajibikaji unaozingatia wakati, weledi, matokeo, ubora, haki, tija na ufanisi katika suala zima la utoaji na upatikanaji wa huduma bora kwa Watu wenye Ulemavu. Matumizi mazuri ya rasilimali

kwa maslahi mapana ya jamii ya Watu wenye Ulemavu kwa ujumla ni lazima yazingatiwe.

### (b) Utii

Wadau wote wanapaswa kuhakikisha kunakuwepo na Utii wa Sheria na Mamlaka husika katika ngazi na hatua zote za utekelezaji wa majukumu yao kwa kufuata na kuheshimu taratibu zilizowekwa.

### (c) Uwazi

Wadau wote wanapaswa kuzingatia utendaji kazi kwa uwazi wakati wote na kuutambua kama jambo la msingi la kufanikisha shughuli zao za utoaji na upatikanaji wa huduma bora kwa Watu wenye Ulemavu nchini. Wadau ni lazima wawe na mifumo inayozingatia uwazi katika utendaji, uandaaji na utoaji wa taarifa za utendaji na zinazohusu vyanzo na matumizi ya fedha pamoja na shughuli zao zote kwa wakati stahiki.

### (d) Utu

Kila Mdau atambue, aheshimu na kuthamini utu wa Watu wenye Ulemavu na Wadau wengine, kama ilivyo wajibu kwa Watu wenye Ulemavu dhidi ya Wadau na Watu wanaowahudumia.

### (e) Ushirikiano

Ili kuimarisha utoaji na upatikanaji wa huduma bora kwa Watu wenye Ulemavu nchini, ni lazima kuwe na ushirikiano wa hali ya juu miongoni na baina ya Wadau wote wa Sekta ya Umma, Binafsi na Asasi za Kiraia. Kila mmoja ajione ni mmiliki na mshiriki wa hatua zote za upangaji na utekelezaji wa Afua

mbalimbali kwa ajili ya kuimarisha ujumuishwaji wa huduma kwa Watu wenye Ulemavu kwa kuzingatia haki na usawa kwa wote.

### (f) Ushirikishwaji wa Wadau

Kila Mdau anapaswa kuhakikisha kuwa anawashirikisha Wadau wengine muhimu katika hatua zote za Mipango, Bajeti, Utekelezaji na Tathmini ya Afua na Shughuli zake kwa ujumla. Ushirikishwaji huu ni lazima uwe kwa uwazi na ujumuishe Mamlaka za Serikali, Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu, Vyama husika vya Watu wenye Ulemavu na Watu wenye Ulemavu wenyewe ambao ndio wanufaika wa Afua na Programu za Mdau katika eneo na ngazi husika. Mamlaka katika maeneo na ngazi husika ni lazima zishirikishwe ili kuwa na taarifa ya kinachofanyika kwenye maeneo yao na kurahisisha usimamizi, uratibu, ufuatiliaji, utoaji taarifa na tathmini ya shughuli za Wadau.

## 3.2. Maeneo Makuu ya Vipaumbele vya Utekelezaji, Ujumuishwaji na Uimarishaji wa Usawa, Haki, Fursa na Huduma kwa Watu wenye Ulemavu

Maeneo makuu saba ya vipaumbele vya kujielekeza kimkakati yalibainishwa baada ya kukusanya na kuchambua maoni na mapendekezo ya Wadau kuhusu hali ya utekelezaji, ujumuishaji, utoaji na upatikanaji wa huduma kwa Watu wenye Ulemavu nchini. Changamoto mbalimbali zilizopo, ikiwemo uwepo wa Afua, Shughuli na Vitendo visivyokidhi mahitaji na maslahi halisi ya Watu wenye Ulemavu miongoni mwa baadhi ya Wadau yalizingatiwa.

Aidha, Wadau wote wanapaswa kuchagua maeneo ya kuyatekeleza kulingana na mamlaka zao za kisera na

kisheria, dhima na maudhui ya shughuli zao. Maeneo haya yatawasaidia kujiwekea malengo mahususi, shabaha, mikakati, shughuli kuu na bajeti ya shughuli na programu zinazopaswa kutekelezwa nao kwa wakati husika kulingana na mahitaji yao na yale ya walengwa na/au wanufaika wao.

Maeneo hayo makuu ya vipaumbele ni ***Utafiti*, *Taarifa* na *Takwimu kuhusu Watu wenye Ulemavu***; ***Ufikivu wa Miundombinu, Usafiri wa Umma, Habari na Mawasiliano kwa Watu wenye Ulemavu****;* ***Huduma za Afya na Ustawi kwa Watu wenye Ulemavu****;* ***Huduma za Elimu, Ujuzi na Mafunzo ya Stadi za Kazi****;* ***Mafunzo ya Stadi za Maisha, Ajira, Kazi za Staha, Hifadhi ya Jamii, Uwezeshaji na Ushirikishwaji Kiuchumi kwa Watu wenye Ulemavu****;* ***Haki na Ulinzi wa Kisheria****; na* ***Ushiriki na Ushirikishwaji wa Watu wenye Ulemavu katika Nyanja mbalimbali za Kijamii na Kisiasa****.*

Maeneo makuu yaliyobainishwa yanaweka na kutoa mwelekeo utakaosaidia wadau wote katika sekta na ngazi mbalimbali; ili waweze kujenga mazingira muafaka kwa Watu wenye Ulemavu Tanzania Bara kujiletea maendeleo; na kutumia vema rasilimali na fursa zilizopo katika kuboresha huduma kwa njia mbalimbali zenye viwango na mwelekeo ulio jumuishi na rahisi kuratibiwa na kusimamiwa kwa kuzingatia matakwa ya Sera, Sheria na Miongozo mingine mbalimbali ya Serikali.

Wadau wanahimizwa kushirikiana na Serikali ili kutekeleza vipaumbele hivi na wanao uhuru wa kuchagua maeneo ya vipaumbele watakayojielekeza katika kutekeleza majukumu na shughuli mbalimbali, kwa kuzingatia mamlaka na nafasi zao kisera na kisheria, kwa lengo la kuimarisha ujumuishaji na huduma kwa Watu wenye Ulemavu.

Ili kuleta matokeo chanya na makubwa zaidi kwa kuzingatia lengo la Kitaifa la kuhakikisha Watu wenye Ulemavu wanapatiwa huduma bora na wanajengewa mazingira wezeshi ya kujitegemea kiuchumi, inapendekezwa vipaumbele hivi vizingatiwe na kila Mdau pindi wanapoandaa mipango mikakati yao ya Utekelezaji, Ujumuishaji na Uimarishaji wa Huduma kwa Watu wenye Ulemavu.

### 3.2.1. Eneo la Kwanza la Kipaumbele: Utafiti, Takwimu na Ukusanyaji wa taarifa kuhusu Watu wenye Ulemavu

Utafiti, taarifa sahihi na takwimu ni nyenzo muhimu katika upangaji na utoaji wa huduma kwa watu wote wakiwemo Watu wenye Ulemavu. Uwepo wa tafiti na takwimu zinazohusiana na masuala ya Watu wenye Ulemavu utawezesha uandaaji wa Sera na Mipango yenye ushahidi wa msingi wa kusaidia utambuzi wa haki na mahitaji halisi ya Watu wenye Ulemavu.

Mwongozo huu unaweka mambo ya msingi ya kuzingatiwa yenye lengo la kuhakikisha taarifa na takwimu sahihi za Watu wenye Ulemavu zinakuwepo. Vilevile, unaweka utaratibu utakaohamasisha Wadau wote wa ndani na nje ya nchi washiriki kikamilifu katika kufanya tafiti stahiki katika eneo hili la huduma.

Hivyo, Wadau husika wanaelekezwa kuzingatia na kutekeleza yafuatayo:

(a) Kuainisha na kuweka maeneo ya kipaumbele ya tafiti kitaifa kuhusu masuala ya Watu wenye Ulemavu kwa matumizi ya umma na watoa huduma kwa kuzingatia

maeneo ya vipaumbele vya kimkakati yaliyomo kwenye Mwongozo huu;

(b) Kufanya tafiti mbalimbali za kina kuhusu ustawi wa Watu wenye Ulemavu;

(c) Kusambaza matokeo na taarifa zitokanazo na takwimu hizi na kuhakikisha kuwa zinapatikana bila vikwazo kwa Watu wenye Ulemavu na wengineo;

(d) Kukusanya taarifa na takwimu za Watu wenye Ulemavu kwa kuzingatia mchanganuo wa aina za ulemavu, jinsi, umri, kiwango cha elimu, hali ya maisha kiuchumi na vigezo vinginevyo;

(e) Kuandaa Mfumo wa Kielektroniki wa Taarifa na Takwimu za Watu wenye Ulemavu unaofikika kwa urahisi kwa umma;

(f) Kuweka taarifa na takwimu katika Mfumo Fikivu kwa Watu wenye Ulemavu wa aina zote;

(g) Kuingiza na kuhuisha masuala ya Watu wenye Ulemavu kwenye kila nyenzo ya ukusanyaji taarifa na takwimu kwenye nyanja zote za Sekta mbalimbali; na

(h) Kuwezesha upatikanaji wa fedha na msaada wa kitaalamu kwa Wadau na Taasisi za Elimu na Utafiti ili kufanya utafiti wenye uhusiano na masuala ya Watu wenye Ulemavu.

### 3.2.2. Eneo la Pili la Kipaumbele: Ufikivu wa Miundombinu, Usafiri wa Umma, Habari na Mawasiliano kwa Watu wenye Ulemavu

Ufikivu wa miundombinu, usafiri wa umma, habari na mawasiliano ni mojawapo ya nyenzo muhimu kwa Watu wenye Ulemavu katika kutimiza haki zao na kujumuishwa kwenye jamii. Aidha, wanayo haki ya kuishi kwa kujitegemea na kushiriki kikamilifu katika nyanja zote za maisha. Kufanikisha haya, Serikali inachukua hatua mbalimbali ili kuboresha mazingira ya ujumuishwaji na upatikanaji wa huduma bora kwa Watu wenye Ulemavu. Hatua hizi ni pamoja na kutunga Sera, Sheria na Miongozo ambayo inalenga kuwahakikishia Watu wenye Ulemavu fursa ya ufikivu wa majengo na huduma mbalimbali za umma; upatikanaji wa huduma kwa usawa na upatikanaji wa taarifa, mawasiliano na habari katika mfumo rahisi.

Katika kuhakikisha kwamba Watu wenye Ulemavu wanaishi kwa kujitegemea na kushiriki kikamilifu katika nyanja zote za maisha, Wadau wanaelekezwa kuzingatia na kutekeleza yafuatayo:

#### 3.2.2.1. Matumizi ya Majengo ya Umma, Barabara, Usafiri na Vifaa vingine

(a) Kuchukua hatua zinazofaa ili kuhakikisha kwamba Watu wenye Ulemavu, wanafika kwenye mazingira yaliyosanifiwa, wanawekewa mfumo rafiki wa usafiri, habari na mawasiliano ikiwa ni pamoja na mifumo na teknolojia ya habari, vifaa na huduma nyinginezo zilizo wazi na zitolewazo kwa umma mijini na vijijini;

(b) Uainishaji na uondoshaji wa mikingamo dhidi ya ufikivu na matumizi ya majengo, barabara, usafiri na vifaa vingine, nje na ndani ya majengo ya huduma kwa umma;

(c) Kufanya marekebisho ya miundombinu iliyopo ikiwa ni pamoja na majengo ili yaweze kutumiwa kwa urahisi na Watu wenye Ulemavu;

(d) Kuhakikisha kwamba wajenzi, wahandisi na wataalamu wengine wa ujenzi wa miundombinu wana uelewa wa kutosha juu ya mahitaji halisi ya Watu wenye Ulemavu kama inavyoelekezwa na Sera, Sheria na Miongozo mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa;

(e) Kuhakikisha kuwa mahitaji ya Watu wenye Ulemavu yanazingatiwa kikamilifu wakati wa utayarishaji wa ramani za majengo;

(f) Kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya kuegesha magari au vyombo vingine vya usafiri vinavyotumiwa na Watu wenye Ulemavu karibu na majengo na milango mikuu ya kuingia ndani ya jengo la huduma kwa umma ili kurahisisha ufikivu wa Watu wenye Ulemavu;

(g) Kuendeleza, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa viwango na miongozo kuhusu ufikivu na upatikanaji wa huduma za umma; na

(h) Kuhakikisha uwepo wa sehemu za huduma za kibinadamu na kijamii maalumu kwa ajili ya Watu wenye Ulemavu katika maeneo yote ya huduma za umma.

**3.2.2.2. Upatikanaji wa Habari, mawasiliano na huduma nyingine ikijumuisha huduma za kielektroniki**

(a) Kuweka ndani ya majengo na sehemu nyingine zinazohudumia umma alama kwa maandishi ya “braille”

na kwa njia nyingine zinazosomeka na kueleweka kirahisi kwa Watu wenye Ulemavu;

(b) Kutoa vifaa saidizi, wasaidizi, waongozaji, wasomaji na wakalimani wa njia zote za mawasiliano kulingana na aina za ulemavu ili kuwawezesha Watu wenye Ulemavu kuyafikia na kuyatumia majengo na huduma nyinginezo za umma;

(c) Kuhamasisha upatikanaji wa aina mpya za teknolojia na mifumo ya habari na mawasiliano, kwa ajili ya Watu wenye Ulemavu;

(d) Kusanifu, kuendeleza, kuzalisha na kusambaza teknolojia na mifumo ya habari na mawasiliano ili zipatikane kiurahisi na kwa gharama nafuu kwa Watu wenye Ulemavu;

(e) Kuongeza uelewa, elimu, ujuzi na maarifa ya upatikanaji na utumiaji wa huduma za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa Watu wenye Ulemavu,

(f) Kurasimisha na kuwezesha matumizi ya lugha ya alama, maandishi ya “braille”, nyenzo za kukuza mawimbi ya sauti na mawasiliano mbadala na aina nyinginezo zinazofikika, mifumo na aina za mawasiliano watakayotumia Watu wenye Ulemavu katika mawasiliano rasmi;

(g) Kuhakikisha huduma za vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, zinafikiwa kiurahisi na Watu wenye Ulemavu;

(h) Kuhakikisha huduma zinazotolewa kwa umma zinatoa habari katika mifumo itayowawezesha Watu wenye Ulemavu kuzifikia na kuzitumia kiurahisi; na

(i) Kuwashirikisha na kuwamasisha Watu wenye Ulemavu kushiriki katika kila hatua ya maendeleo na matumizi ya TEHAMA.

### 3.2.3. Eneo la Tatu la Kipaumbele: Afya na Ustawi wa Jamii kwa Watu wenye Ulemavu

Sekta za Afya na Ustawi wa Jamii ni muhimu kwa maendeleo ya Watu wenye Ulemavu. Sekta hizi zinajumuisha miundombinu, wataalamu, vifaa saidizi, vifaa tiba, vitendanishi, dawa, huduma za tiba, marekebisho, utengamao, kinga, msaada wa kisaikolojia na kijamii, misaada ya kijamii ya dharura na bima ya afya. Huduma hizi zote zinapaswa kuwa jumuishi, fikivu na zinazozingatia haki stahiki na mahitaji halisi ya Watu wenye Ulemavu.

Hivyo, Wadau husika wanaelekezwa kuchukua hatua madhubuti katika eneo hili kwa kuzingatia na kutekeleza mambo yafuatayo:

#### 3.2.3.1. Afya

(a) Kutambua na kuhakikisha kwamba Watu wenye Ulemavu wanapata haki ya kunufaika na huduma za afya bila ya ubaguzi wa aina yoyote;

(b) Kuhuisha na kuandaa mitaala ya elimu ya huduma za afya inayozingatia mahitaji ya Watu wenye Ulemavu;

(c) Kutoa mafunzo kwa watumishi wa sekta ya afya ili kuongeza ufahamu wa masuala ya haki za binadamu, hadhi, uhuru, mawasiliano na mahitaji ya Watu wenye Ulemavu;

(d) Kuhakikisha kwamba Watu wenye Ulemavu wanapatiwa matibabu na aina mbalimbali za huduma za afya, ikiwemo bima ya afya isiyo na mipaka au huduma za afya bila ya malipo kwa wasio na uwezo, vifaa saidizi na vifaa tiba kwa ubora na viwango stahiki kulingana na mahitaji halisi yanayozingatia aina za ulemavu walionao na viwango vya maadili ya kitabibu;

(e) Kuwajengea uwezo watumishi wote wa sekta ya afya na jamii kwa ujumla kwa njia ya mafunzo katika maeneo ya utambuzi wa mapema, afua stahiki, uzuiaji wa mapema wa ulemavu na upunguzaji wa madhara yake;

(f) Kuwezesha utoaji na upatikanaji wa taarifa za huduma za afya katika mifumo fikivu na rafiki kwa Watu wenye Ulemavu; ikiwemo kwa njia mbalimbali za mawasiliano kulingana na mahitaji ya aina za ulemavu walio nao, katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya nchini; na

(g) Kuongeza uwakilishi wa Watu wenye Ulemavu kwenye vyombo vya ushauri wa masuala ya afya kwa wote.

### 3.2.3.2. Ustawi wa Jamii

(a) Kuhamasisha, kuwezesha na kufanya utambuzi wa mapema; na kutekeleza afua stahiki na huduma zenye lengo la kuzuia na kupunguza ulemavu zaidi miongoni mwa watoto na watu wazima, zikiwemo huduma za marekebisho na utengamao;

(b) Kutoa mafunzo kwa watumishi wa sekta mbalimbali ili kuongeza ufahamu wa masuala ya haki za binadamu, hadhi, uhuru, mawasiliano na mahitaji ya Watu wenye Ulemavu;

(c) Kuhakikisha kwamba Watu wenye Ulemavu wanapatiwa matibabu na aina mbalimbali za huduma za afya, ikiwemo bima ya afya isiyo na mipaka au huduma za afya bila ya malipo kwa wasio na uwezo, vifaa saidizi na vifaa tiba kwa ubora na viwango stahiki kulingana na mahitaji halisi yanayozingatia aina za ulemavu walionao na viwango vya maadili ya kitabibu;

(d) Kuhakikisha kwamba Watu wenye Ulemavu wanapatiwa huduma ya msaada wa kisaikolojia na kijamii; mahitaji ya msaada wa dharura kwa utaratibu wa kawaida na wakati wa majanga;

(e) Kuandaa programu za kuelimisha na kuhamasisha umma ili kupunguza vyanzo na madhara ya ulemavu katika nyanja na Sekta mbalimbali nchini.

#### 3.2.3.3. Marekebisho na Utengamao

(a) Kuandaa, kuimarisha na kupanua huduma za marekebesho na utengamao, hususani katika nyanja za afya, elimu na huduma za kijamii;

(b) Kuimarisha na kupanua wigo wa huduma za upimaji ili kuwafikia Watu wenye Ulemavu katika maeneo yaliyo karibu na jamii zao;

(c) Kuendesha Mafunzo ya Marekebisho na Huduma za Utengamao kwa Watu wenye Ulemavu;

(d) Kutoa mafunzo kwa ajili ya wataalamu na watumishi wanaofanyakazi katika fani za marekebisho na utengamao na kuongeza idadi yao ili kukidhi mahitaji;

(e) Kuhakikisha upatikanaji wa maarifa, matumizi ya vifaa saidizi na teknolojia iliyosanifiwa kwa ajili ya Watu wenye Ulemavu kuhusiana na huduma za marekebisho na utengamao;

(f) Kuimarisha na kuhamasisha utoaji, uendeshaji, usimamizi na uratibu wa Huduma za Marekebisho za Kijamii; na

(g) Kuandaa na kutekeleza mfumo utakaowezesha watoa huduma za umma na binafsi kutoa Huduma za Marekebisho na Utengamao ndani ya jamii.

#### 3.2.3.4. Utoaji wa Nyenzo za Kujimudu

(a) Kuhakikisha Watu wenye Ulemavu wanapata nyenzo bora za kujimudu ikijumuisha vifaa na teknolojia saidizi; pamoja na aina nyingine ya usaidizi kwa gharama nafuu na/au kwa njia ya msaada;

(b) Kuhakikisha vifaa saidizi vilivyo bora vinazalishwa hapa nchini, na kwa bei nafuu kwa ajili ya Watu wenye Ulemavu; na

(c) Kuandaa programu za kuelimisha na kuhamasisha umma matumizi sahihi ya nyenzo za kujimudu.

### 3.2.4. Eneo la Nne la Kipaumbele: Ubora wa Elimu, Ujuzi, Stadi za Kazi na Stadi za Maisha

Watu wenye Ulemavu wana haki ya kupata elimu, ujuzi na mafunzo katika mifumo jumuishi na fikivu. Huduma hizi humpa nafasi Mtu Mwenye Ulemavu na njia ya kujiendeleza, kupata ajira, kutawala mazingira kwa maendeleo yake na kufikia ujumuishwaji ulio timilifu katika jamii. Hatua mbalimbali

zimechukuliwa na Serikali katika kuboresha kiwango na ushiriki wa Watu wenye Ulemavu katika huduma za elimu, ujuzi na mafunzo ya stadi za kazi. Hatua hizo ni pamoja na huduma za utengamao na marekebisho, uboreshaji wa ufikivu wa miundombinu, utoaji wa vifaa saidizi, vifaa vya kujifunzia na kufundishia; na uongezaji na uimarishaji wa Afua za utambuzi na udahili wa Watoto wenye Ulemavu wenye umri wa kwenda shule.

Hata hivyo, jitihada zaidi zinahitajika kuimarisha huduma za elimu katika ngazi zote, kuanzia elimu ya awali, msingi, sekondari na vyuo vya elimu ya kati na juu, kwa kuzingatia mahitaji maalumu ya Watu wenye Ulemavu. Kwa muktadha huu, Wadau husika wanaelekezwa kuchukua hatua madhubuti ili kuongeza tija, ufanisi, ujumuishwaji na ushindani wa Watu wenye Ulemavu katika Sekta ya Elimu ili kuleta maendeleo yao binafsi na taifa kwa ujumla. Mambo ya kuzingatiwa na kutekelezwa na Wadau husika ni yafuatayo:

#### 3.2.4.1. Ubora wa Elimu

(a) Kuwezesha uingizwaji wa elimu ya masuala ya ulemavu kwenye mitaala na mifumo ya elimu katika ngazi zote;

(b) Kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia na kuyafanya yawe jumuishi katika ngazi zote za utoaji wa elimu, ikiwemo njia za mawasiliano na huduma za ufikivu;

(c) Kuboresha na kuwianisha idadi ya watumishi, wataalamu wa elimu maalumu na elimu jumuishi, pamoja na zana na vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu;

(d) Kuboresha miundombinu ya Taasisi za Elimu katika ngazi zote ili kukidhi mahitaji ya Watu wenye Ulemavu;

(e) Kuhuisha na kuandaa mitaala inayozingatia mahitaji ya elimu na ujuzi kwa Watu wenye Ulemavu na soko la ajira;

(f) Kuhuisha na kufungamanisha mafunzo ya nadharia na vitendo ili iweze kuzingatia mahitaji ya Watu wenye Ulemavu na soko la ajira;

(g) Kuhakikisha upatikanaji wa huduma muhimu za kuwawezesha Watu wenye Ulemavu kujumuishwa katika ngazi zote za huduma za elimu, ikiwemo kupatiwa huduma za ushauri wa kisaikolojia, mikopo nafuu, misaada kwa njia ya ruzuku na huduma nyinginezo stahiki;

(h) Kuhakikisha uwepo wa mafunzo ya njia zote za mawasiliano ambapo kuna Watu wenye Ulemavu na kuwezesha huduma za ushauri katika makundi rika;

(i) Kuhakikisha uwepo wa huduma za utoaji wa ruzuku kwa elimu ya juu kwa Wanafunzi wenye Ulemavu au ambao wazazi wao ni Watu wenye Ulemavu wasio na uwezo wa kugharamia huduma za elimu ya juu;

(j) Kuhakikisha Watu wenye Ulemavu wananufaika na elimu mbadala kuwawezesha kumudu mazingira ya kujiajiri na kuajiriwa;

(k) Kuhakikisha kuwa njia za utahini (mitihani na mazoezi) zinazingatia hali ya ulemavu wa mwanafunzi husika;

(l) Kuhakikisha uwepo wa wasaidizi kwa Wanafunzi wenye Ulemavu ulio wa kiwango kikubwa wasioweza kujimudu;

(m) Kuhakikisha Programu ya utambuzi wa mapema wa ulemavu kwa Watoto walio mashuleni inatekelezwa kikamilifu; na

(n) Kuhamasisha utoaji motisha za aina mbalimbali kwa Taasisi za Elimu zinazopiga hatua na kufanya vema katika elimu jumuishi kwa ajili ya Watu wenye Ulemavu.

#### 3.2.4.2. Ujuzi, Stadi za Kazi na Stadi za Maisha

(a) Kuongeza na kuboresha miundombinu katika Ujuzi na Stadi za Kazi ili ziweze kudahili na kutoa mafunzo kwa kuzingatia mahitaji ya Watu wenye Ulemavu wa aina zote;

(b) Kuongeza udahili wa Watu wenye Ulemavu katika Taasisi za Elimu na Mafunzo kwa fani zote kulingana na mahitaji ya aina ya ulemavu alionao;

(c) Kuanzisha, kuimarisha na kuendeleza programu za mafunzo kwa vitendo mahali pa kazi kabla ya ithibati; na mafunzo ya kujiendeleza katika fani jumuishi na maalumu kwa ajili ya Watu wenye Ulemavu, utakaowawezesha kupata uzoefu wa kujiajiri na kuajirika kirahisi;

(d) Kuhamasisha ubunifu na uhawilishaji wa ujuzi na teknolojia miongoni mwa Watu wenye Ulemavu;

(e) Kuhamasisha Watu wenye Ulemavu juu ya umuhimu wa elimu, ufundi, ujuzi wa stadi za kazi, stadi za maisha na ujasiriamali katika kujiinua kiuchumi; na

(f) Kuanzisha, kusimamia na kutekeleza utaratibu wa kutoa zana za kuanza kazi kwa Watu wenye Ulemavu wanaohitimu mafunzo ya ufundi na ujuzi wa stadi za kazi na kuwawezesha kimtaji.

### 3.2.5. Eneo la Tano la Kipaumbele: Ajira, Kazi za Staha, Kinga na Hifadhi ya Jamii, Uwezeshaji na

### Ushirikishwaji Kiuchumi kwa Watu wenye Ulemavu

Uboreshaji wa maisha kwa Watu wenye Ulemavu nchini ni pamoja na kuhakikisha kuwa wanajumuishwa katika huduma za Hifadhi ya Jamii, Uwezeshaji Kiuchumi, Ushirikishwaji katika shughuli mbalimbali za uzalishaji mali zenye staha; na kuboresha mazingira ya upatikanaji wa huduma anuwai za kupunguza umaskini wa kipato, ikiwemo kuwapatia fursa za ajira na kuwajengea uwezo wa kupambana na mazingira yanayowazunguka ili kujitegemea na kukuza mchango wao katika maendeleo yao binafsi na jamii kwa ujumla.

Wadau wa usimamizi na utoaji wa huduma hizo wana wajibu mkubwa wa kuhakikisha zinawafikia Walengwa wenye Ulemavu kwa ubora na viwango stahiki kulingana na mahitaji ya aina za ulemavu walionao. Kufanikisha hili, Wadau husika wanaelekezwa kuzingatia na kutekeleza mambo yafuatayo:

#### 3.2.5.1. Upatikanaji wa Mitaji, Masoko, Elimu ya Biashara na Ujasiriamali kwa Watu wenye Ulemavu

(a) Kufanya utafiti na kutathmini hali ya uwezeshaji na ushirikishwaji kiuchumi kwa Watu wenye Ulemavu na familia zao na kupendekeza njia za uboreshaji;

(b) Kuandaa, kusimamia na kuratibu Programu za uwezeshaji na ushirikishwaji kiuchumi kwa Watu wenye Ulemavu;

(c) Kuandaa, kusimamia na kuratibu utengaji wa maeneo jumuishi kwa ajili ya shughuli za kiuchumi na kijamii kwa Watu wenye Ulemavu;

(d) Kutoa huduma za uendelezaji wa biashara kwa Watu wenye Ulemavu;

(e) Kuwawezesha Watu wenye Ulemavu kushiriki katika shughuli za ujasiriamali, ikiwemo kuwapatia mafunzo na kuwaunganisha na Taasisi na Asasi za utoaji mikopo yenye riba na masharti nafuu;

(f) Kuwawezesha na kuwashirikisha Watu wenye Ulemavu wanaohitimu elimu ya juu na vyuo vya ufundi; vyuo vya ufundi stadi na marekebisho na ujuzi kuunda vikundi na makampuni kwa lengo la kuwapatia mitaji na nyenzo kupitia Taasisi za Fedha, Programu na Mifuko ya Uwezeshaji;

(g) Kuweka mfumo ambao utawawezesha Watu wenye Ulemavu, walio katika vikundi au mtu mmoja mmoja, kufanya shughuli za ujasiriamali na kuwaunganisha na fursa za upatikanaji wa mitaji na masoko;

(h) Kuhamasisha na kuwajengea uwezo wa ushiriki wa Watu wenye Ulemavu katika kupata zabuni kama inavyoelekezwa katika Sheria ya Manunuzi; na

(i) Kubuni na kutekeleza mikakati ya kuhakikisha kuwa elimu ya ujasiriamali inayotolewa na wadau mbalimbali ikiwemo Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia ina ubora unaokidhi mahitaji ya Watu wenye Ulemavu.

### 3.2.5.2. Ajira na Kazi za Staha

(a) Kulinda na kukuza haki ya kuajiriwa, kujiajiri, kuajiri na kufanya kazi kwa Watu wenye Ulemavu, ikijumuisha wale wanaopata ulemavu wakiwa kazini;

(b) Kuhamasisha na kukuza fursa za Watu wenye Ulemavu kujiajiri wenyewe, kuanzisha na kuendesha shughuli za ujasiriamali, kuanzisha vyama vya ushirika na mtu binafsi kujianzishia biashara zake;

(c) Kuwezesha na kuongeza fursa za ajira, kuajiri na kupandisha madaraja Watu wenye Ulemavu, pamoja na kuwapatia huduma za usaidizi wa aina mbalimbali, ikiwemo ulinzi na usalama wa ajira na kurejeshwa kazini baada ya huduma ya utengemao;

(d) Kuchukua hatua stahiki ili kupiga vita vitendo vya ubaguzi, unyanyasaji na udhalilishaji mahala pa kazi na ajira kwa msingi wa ulemavu, jinsi au vinginevyo; ikiwemo kuweka masharti bayana, stahiki na fikivu; taratibu na mazingira jumuishi na shirikishi katika njia na mbinu za kutangaza nafasi za ajira, wakati wa usaili, kuchagua na kuajiri; kudumu kazini, upandishwaji vyeo na madaraja; na mazingira ya kazi yaliyo salama kiafya;

(e) Kuwezesha Watu wenye Ulemavu kutumia haki zao mahali pa kazi na katika Vyama vya Wafanyakazi kwa misingi ya uhuru na usawa;

(f) Kuwezesha Watu wenye Ulemavu kuzifikia na kunufaika na programu zinazohusiana na maendeleo ya teknolojia, kupata uzoefu, ushauri wa kiufundi, huduma za mafunzo kazini, utambuzi, urasimishaji na uendelezaji ujuzi;

(g) Kuwezesha utoaji na uimarishaji wa huduma za kiajira na kazi kwa Watu wenye Ulemavu katika Utumishi wa Umma na Sekta Binafsi; ikiwa ni pamoja na kutenga nafasi za kazi kwa mujibu wa Sheria kwa ajili ya Watu wenye Ulemavu kulingana na mahitaji ya aina

mbalimbali za ulemavu walionao na kutoa tuzo/motisha kwa Waajiri na Waajiriwa wanaofanya vema;

(h) Kuhakikisha kwamba huduma za utengamao na marekebisho stahiki yanafanyika mahali pa kazi kwa ajili ya Watu wenye Ulemavu;

(i) Kupiga vita vitendo vya usafirishwaji na utumikishwaji haramu; kazi za shuruti, unyanyasaji na unyonyaji dhidi ya Watu wenye Ulemavu na kuwahakikishia ulinzi, afya na usalama mahala pa kazi na ajira;

(j) Kuepuka kuongeza masharti ya ziada ambayo si ya lazima katika matangazo ya nafasi za ajira yenye kuweza kusababisha na kuleta hofu kwa waombaji wenye Ulemavu na kuchukua hatua mahususi ili kuongeza fursa kwao, kuwajumuisha na kuwafikia kiurahisi;

(k) Kuhakikisha taarifa zinazotolewa kuhusu fursa za ajira zinahamasisha Watu wenye Ulemavu kuchangamkia fursa ya kuomba ajira kama inavyoelekezwa katika Sheria ya Watu wenye Ulemavu; na

(l) Kuwezesha majadiliano ya kina na Watu wenye Ulemavu, namna ulemavu wao unavyoweza kuathiri utendaji wa kazi zao na mahitaji halisi ya kurekebisha na kuondoa vikwazo ili waweze kuajiriwa na kufanya kazi kwa tija na ufanisi kwa kadri ipasavyo.

### 3.2.5.3. Kinga na Hifadhi ya Jamii

(a) Kuweka mazingira wezeshi yanayotambua na kulinda haki ya Watu wenye Ulemavu kupata huduma za

hifadhi ya jamii na kufaidika na haki hiyo bila ya ubaguzi wa aina yoyote;

(b) Kuhakikisha huduma stahiki za kijamii zikijumuisha visaidizi na usaidizi zinawafikia Watu wenye Ulemavu na zinakuwa zenye gharama nafuu au bila malipo;

(c) Kuhakikisha kwamba huduma ya hifadhi ya jamii na ile ya kupunguza umasikini inawafikia Watu wenye Ulemavu, ikiwemo kutoa ruzuku kwa Watu wenye Ulemavu wasiojiweza na wasiojimudu;

(d) Kuwezesha upatikanaji wa huduma mahususi kwa Watu wenye Ulemavu na familia zao wanaoishi katika hali ya umasikini mkubwa, ikiwemo elimu, mafunzo, ushauri nasaha, ruzuku, huduma za chakula, afya, ulinzi, usalama, makazi na matunzo wakati wa fadhaa zinazotokana na ulemavu, dharura za milipuko na majanga ya kiasili; na

(e) Kuwezesha upatikanaji wa huduma za ziada kwa Mfumo wa Hifadhi ya Jamii kwa Watu wenye Ulemavu.

### 3.2.6. Eneo la Sita la Kipaumbele: Haki na Ulinzi wa Kisheria

Watu wenye Ulemavu, kama ilivyo kwa wananchi wengine, wanayo haki ya kuheshimiwa, kutobaguliwa na kuthaminiwa utu wao. Wadau wanapaswa kuhakikisha uwepo na upatikanaji wa haki na ulinzi stahiki wa kisheria kwa Watu wenye Ulemavu katika misingi ya usawa na watu wengine.

Hivyo, ili kuwahakikishia Watu wenye Ulemavu huduma za upatikanaji wa haki na ulinzi wa kisheria nchini, Wadau husika wanaelekezwa kuzingatia na kutekeleza mambo yafuatayo: -

### 3.2.6.1. Kukuza Uelewa kuhusu Sera, Sheria na Miongozo

(a) Kukuza ufahamu katika jamii yote, ikiwemo ndani ya familia kuhusu dhana ya ulemavu, huduma zilizopo kwa ajili ya Watu wenye Ulemavu na kuendeleza na kuwahakikishia heshima, haki za msingi za kibinadamu, thamani na hadhi ya utu wao;

(b) Kupambana mtazamo hasi ndani ya jamii, ikiwemo ukatili na mienendo yenye madhara dhidi ya Watu wenye Ulemavu na ile yenye kuegemea jinsi na umri katika nyanja zote za maisha;

(c) Kuanzisha na kuendeleza kampeni zinazolenga kuendeleza haki za kiraia kwa Watu wenye Ulemavu zinatambulika, kuheshimiwa na kutekelezwa ipasavyo katika jamii, ikiwemo kutoa huduma za ushauri na msaada wa kisheria;

(d) Kuondoa vizuizi vya kijamii vinavyozuia Watu wenye Ulemavu kushiriki katika ufikiaji wa huduma za upatikanaji haki za Kikatiba na ulinzi wa kisheria kama raia wengine wasio na ulemavu;

(e) Kuhakikisha kamati mbalimbali zinazoundwa kwa mujibu wa sheria ya msaada wa kisheria zinajumuisha Watu wenye Ulemavu; na

(f) Kuimarisha, kutekeleza, kuratibu na kusimamia Mfumo thabiti wa Kisera na kisheria unaowahakikishia Watu

wenye Ulemavu haki, ulinzi na usalama katika maisha na upatikanaji wa huduma za msingi na ziada.

### 3.2.6.2. Utoaji wa Haki na Fursa Sawa kwa Watu wenye Ulemavu

(a) Kutambua kwamba watu wote ni sawa mbele ya sheria na wanastahili kulindwa na kunufaika na sheria kwa usawa bila ya ubaguzi wowote;

(b) Kupinga aina zote za ubaguzi kwa misingi ya ulemavu na kubeba dhamana ya kuhakikisha kwamba, Watu wenye Ulemavu wanapewa ulinzi sawa na imara wa kisheria dhidi ya ubaguzi na unyanyapaa wa aina yoyote;

(c) Kukuza usawa na kuondoa ubaguzi, kwa kuchukua hatua zinazohitajika ili kuhakikisha kuwa marekebisho yanayostahili yanafanyika kwa wakati muafaka;

(d) Kuchukua hatua za makusudi katika kuharakisha au kufanikisha ufikivu na upatikanaji wa haki na usawa kwa Watu wenye Ulemavu;

(e) Kufanya uelimishaji na uhamasishaji kwa wadau wote wa sekta binafsi na umma wakiwemo Watu wenye Ulemavu juu ya hali, ulinzi, usalama na masuala mengine yanayohusiana na Ulemavu;

(f) Kuhakikisha kuwa vyombo vya utekelezaji wa sheria vinazingatia haki kwa mujibu wa Shera kwa Watu wenye Ulemavu kutumia vifaa saidizi kulingana na mazingira stahiki na usalama;

(g) Kuweka, kusimamia na kutekeleza mikakati madhubuti pamoja na msaada wa kisheria, kisaikolojia na vifaa ili

kuwezesha ushiriki stahiki wa Watu wenye Ulemavu katika kesi na huduma zote za kisheria; na

(h) Kufanya uhamasishaji na uelimishaji kwa Watumishi na Watendaji wa Mahakama, Wataalamu wa Sheria na vyombo vingine vya kisheria, ikiwemo Polisi na Magereza juu ya haki, ulinzi, usalama, dhana na masuala mengine kuhusiana na Watu wenye ulemavu.

#### 3.2.6.3. Usimamizi, Uratibu na Utekelezaji wa Sera, Sheria na Miongozo Mbalimbali

(a) Kuwezesha mapitio na marekebisho ya Sera, Sheria na Miongozo mbalimbali kwa lengo la kutoa haki kwa Watu wenye Ulemavu ili kuendana na mahitaji ya wakati;

(b) Kuchukua hatua mahususi na madhubuti za kisheria, kiutawala, kijamii, kielimu na nyinginezo, ili kuwalinda Watu wenye Ulemavu katika misingi ya usawa na watu wengine, ili wasifanyiwe udhalimu, unyonyaji, unyanyasaji na kudhalilishwa kinyume cha utu na ubinadamu; ikijumuisha, kuzuia aina zote za unyonyaji, utumikishaji wa aina zote ikiwemo katika kuombaomba mitaani, ukatili na udhalilishaji kwa kuhakikisha kunakuwepo mifumo stahiki ya usaidizi inayozingatia jinsi na makundi rika ya Watu wenye Ulemavu, familia na walezi wao;

(c) Kutambua, kusajili, kuratibu na kuwezesha uanzishwaji na uimarishwaji wa shughuli za Vyama, Jumuiya na Asasi za Kiraia na Sekta Binafsi kwa ajili ya kuhudumia Watu wenye Ulemavu katika ngazi zote nchini na kuhakikisha kwamba shughuli zote za ustawi wa Watu wenye Ulemavu zinatekelezwa kwa haki, usawa na uwazi kupitia Vyama, Jumuiya, Asasi mbalimbali na ushirikiano na mashauriano ya Mamlaka za Serikali na Wadau wengine yanafanyika kwa kuzingatia uwakilishi wa Taasisi kuu zilizotambuliwa

na kusajiliwa kisheria kama mwamvuli kwa kila aina ya ulemavu na kudhibiti utitiri wa Taasisi na Asasi zisizo zingatia mwelekeo wa ustawi na maslahi ya Watu wenye Ulemavu;

(d) Kutambua, kuhamasisha, kuchangia, kuwezesha na kushiriki kikamilifu katika uwepo na utekelezaji wa shughuli za maadhimisho ya kitaifa na kimataifa kwa Watu wenye Ulemavu nchini kwa utaratibu kisheria na unaoeleweka bayana na kukubalika kwa Wadau, zikiwemo Mamlaka za Serikali, kwa kuzingatia Maadili ya Msingi ya Mwongozo; na

(e) Kuwezesha na kukuza ushirikishwaji na mashauriano na Wadau wa masuala ya Watu wenye Ulemavu, kupitia vyombo vyao vya uwakilishi rasmi wa kisheria, katika michakato yote ya utungaji, utekelezaji na marekebisho ya Sera, Sheria, Miongozo na michakato mingine ya kufanya maamuzi katika ngazi zote ili kuhakikisha ujumuishwaji wa masuala na haki za Watu wenye Ulemavu.

### 3.2.7. Eneo la Saba la Kipaumbele: Ushiriki na Ushirikishwaji wa Watu wenye Ulemavu katika Nyanja mbalimbali za Kijamii na Kisiasa

Ushiriki na ushirikishwaji wa Watu wenye Ulemavu ni kanuni ya jumla kama ilivyoelezwa bayana kwenye Katiba ya Jamhuri ya Tanzania, Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Watu wenye Ulemavu na Sheria ya Watu wenye Ulemvu. Nyaraka hizo zinatoa wito wa kushiriki kikamilifu, kuwashirikisha na kushauriana kwa karibu na Watu wenye Ulemavu na Vyama vyao katika mambo ya maendeleo na utekelezaji wa Sera na Sheria; na katika michakato mingine ya kufanya maamuzi kuhusu masuala yanayohusiana na Watu wenye Ulemavu na jamii kwa ujumla.

Hivyo, katika kuhakikishia Watu wenye Ulemavu haki ya kushiriki na kushirikishwa kwenye nyanja mbalimbali za kisiasa na kijamii; ikiwemo mambo ya Kitamaduni, Sanaa, Mapumziko, shughuli za Burudani na Michezo, shughuli za kisiasa, ngazi za maamuzi na uwekaji mipango kwa misingi ya usawa na kama ilivyo kwa watu wengine; Wadau husika wanaelekezwa kuzingatia na kutekeleza yafuatayo: -

#### 3.2.7.1. Watu wenye Ulemavu Kushiriki katika Siasa na Kuhudumia Umma

(a) Kuhakikisha kuwa Watu wenye Ulemavu wanashirikishwa kwa ukamilifu katika medani ya siasa na huduma kwa umma kwa misingi iliyo sawa na wengine moja kwa moja au kwa kupitia wawakilishi waliochaguliwa kwa misingi huru kulingana na aina za ulemavu zilizopo, ikiwa ni pamoja na fursa ya Watu wenye Ulemavu kupiga kura ili kuchagua na kuchaguliwa;

(b) Kujenga na kuimarisha mazingira rafiki na fikivu, ambayo Watu wenye Ulemavu wanaweza kushiriki kikamilifu katika masuala ya umma bila vikwazo, na kwa misingi ya usawa na wengine, na kuhimiza ushiriki wao katika mambo ya umma;

(c) Kuhakikisha kuwa Watu wenye Ulemavu wanashirikishwa na kushiriki kwenye uongozi wa Asasi za Kiraia na zile zinazojihusisha na masuala ya huduma kwa umma na siasa za nchi, ikiwemo shughuli na uongozi wa Vyama vya Siasa;

(d) Kuweka na kusimamia mfumo unaowezesha Watu wenye Ulemavu kuunda na kujiunga na Shirikisho na Vyama vya Watu wenye Ulemavu ili kuwawakilisha katika maeneo yao na ngazi za kitaifa, kimataifa na kikanda.

#### 3.2.7.2. Kushiriki katika Masuala ya Kitamaduni, Sanaa, Burudani na Michezo

(a) Kuwezesha uwepo wa mfumo fikivu na rahisi utakaosaidia na kuhamasisha Watu wenye Ulemavu wa aina mbalimbali kupata na kushiriki shughuli na huduma zote za utamaduni, sanaa, burudani na michezo, ikiwemo uanzishwaji wa Sehemu na vitengo mahususi vinavyoshughulikia na kuratibu masuala haya ndani ya Miundo ya Vyama vya Watu wenye Ulemavu, Mamlaka za Tasnia hizo na Wadau wengine;

(b) Kuondoa vikwazo vya kimazingira, kitaasisi, kisera na kisheria ili kuwezesha kufanyika kwa shughuli na huduma jumuishi za michezo, burudani, ubunifu, sanaa na utamaduni kwa Watu wenye Ulemavu, ikiwemo vifaa na utaalamu.

(c) Kuhamasisha na kuwajengea uwezo Watu wenye Ulemavu kupata fursa ya kujiendeleza na kutumia ubunifu, usanii na uwezo wao kiakili, katika kujiletea maendeleo binafsi na jamii nzima;

(d) Kuhakikisha kuwa Watoto wenye Ulemavu wanapata nafasi sawa na wenzao ya kushiriki katika michezo, mapumziko, ubunifu, sanaa na burudani; na shughuli zote za michezo ikijumuisha ile iliyo kwenye mfumo wa kishule; na

(e) Kuwezesha uhuishaji wa Sera, Sheria na Kanuni na kuweka Mipango Mahususi na Jumuishi ili kuhakikisha kuwa Watu wenye Ulemavu wanashirikishwa na kushiriki katika shughuli za kiutamaduni, michezo, sanaa na burudani kitaifa na kimataifa kwa usawa na wengine; na kwamba shughuli hizo kwa Watu wenye Ulemavu

zinakuwa sehemu ya Mipango ya Maendeleo ya Tasnia hizo Kitaifa na Kisekta.

### 3.2.7.3. Ujumuishwaji wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu katika Mipango ya Maendeleo ya Kisekta

a) Kuhakikisha kuwa vipaumbele vya masuala ya huduma kwa Watu wenye Ulemavu vinajumuishwa katika Mipango ya Kisekta na Kitaasisi miongoni mwa Wadau wa Sekta ya Umma na Binafsi;
b) Kuhakikisha na kuwezesha ushirikishwaji na ushiriki wa Watu wenye Ulemavu katika michakato na hatua zote za maandalizi na utekelezaji wa mipango na bajeti ya maendeleo na utekelezaji wa shughuli za kisekta na kitaasisi kupitia miundo ya uwakilishi wao kisheria;

c) Kushiriki katika kuwajengea uwezo Watu wenye Ulemavu katika eneo la uchechemuzi, ushirikishwaji, ushiriki, ujumishwaji, ufuatiliaji na tathmini ili waweze kunufaika ipasavyo katika mipango na programu mbalimbali ya Sekta na Taasisi katika jamii wanayoishi;

d) Kuhamasisha na kuwezesha uanzishwaji na uimarishwaji wa Kamati na Madawati ya Watu wenye Ulemavu kwenye Wizara, Taasisi, Idara, Wakala Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa nchini; na

e) Kuimarisha Usimamizi, Uratibu na Utekelezaji wa Mwongozo huu ili kukuza na kuboresha nafasi ya Watu wenye Ulemavu katika ushiriki kwenye maendeleo yao na nchi kwa ujumla.

# SURA YA NNE

## 4.0. UTEKELEZAJI WA MWONGOZO NA MAJUKUMU YA WADAU

### 4.1. Mfumo wa Utekelezaji wa Mwongozo

Mfumo wa utekelezaji wa Mwongozo unahusisha taratibu za kiutendaji za Serikali na Sekta binafsi. Taratibu hizo zinajumuisha maandalizi ya mipango kazi ya kisekta, kitaasisi na bajeti za utekelezaji wa shughuli na hatua mahsusi zitakazotokana na vipaumbele vilivyoainishwa kwenye mwongozo huu; mtiririko wa mahitaji ya rasilimali muhimu na mipango ya ufuatiliaji na tathmini.

### 4.2. Gharama za Utekelezaji wa Maeneo ya Vipaumbele vya Mwongozo

Gharama za utekelezaji wa maeneo ya vipaumbele yaliyobainishwa na "Mwongozo wa Utekelezaji, Ujumuishwaji na Uimarishaji wa Huduma kwa Watu wenye Ulemavu Tanzania wa mwaka 2022" zinategemewa ziainishwe na kutengewa bajeti kulingana na Mipango, Mikakati na Bajeti za Wadau husika wa utekelezaji, kila mmoja kulingana na mahitaji ya eneo linalomhusu au alilochagua kujielekeza kwa wakati husika.

### 4.3. Matokeo ya Utekelezaji yanayotarajiwa

Matokeo yanayotarajiwa ni kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa ya kuifanya nchi ya Tanzania kuwa na jamii jumuishi inayoongoza katika kuzingatia haki na ustawi kwa wananchi wote kwa usawa; kutambua na kuthamini utu wa

kila mtu, wakiwemo Watu wenye Ulemavu. Elimu itaendelea kutolewa kwa Wadau na Jamii yote; na kuwahamasisha kuhusu umuhimu wa utekelezwaji wa Mwongozo huu ili hatimaye kuweza kupatikana kwa huduma bora kwa Watu wenye Ulemavu ikiwa ni pamoja na kuimarika kwa mifumo ya ujumuishwaji, uratibu, usimamizi, utekelezaji na ufikiwaji wa masuala mbalimbali ya huduma kwa Watu wenye Ulemavu.

## 4.4. Majukumu ya Wadau

Majukumu ya Wadau mbalimbali kuhakikisha Mwongozo huu unatekelezeka kikamilifu kama ulivyokusudiwa ili kuboresha huduma kwa Watu wenye Ulemavu ni ifuatavyo:

### 4.4.1. Wizara yenye Dhamana ya Masuala ya Watu wenye Ulemavu

(a) Kuhakikisha mipango mikakati na mipango kazi ya Wadau wanaokusudia kutoa huduma kwa Watu wenye Ulemavu inazingatia miongozo iliyowekwa kuhudumia Watu wenye Ulemavu;

(b) Uratibu, ufuatiliaji, tathmini na upimaji wa matokeo ya shughuli na programu za Wadau;

(c) Kuhakikisha kuwa vipaumbele, malengo na shughuli zote zilizoainishwa katika Mwongozo huu zinatekelezwa ipasavyo na Wadau wote kwa kuzingatia matakwa mbalimbali ya kisera na kisheria;

(d) Kuweka mazingira wezeshi kisera na kisheria ili kutimiza malengo ya Mwongozo;

(e) Kuimarisha huduma za uratibu na usimamizi pamoja na kufanya ufuatiliaji wa karibu kwa kila mdau kwa kushirikiana na mamlaka nyingine zinazohusika katika ngazi za Mikoa, Wilaya na Halmashauri zote nchini; na

(f) Kusaidia upatikanaji wa vifaa na utaalamu unaohitajika kulingana na maeneo ya utekelezaji wa Mwongozo miongoni mwa Wadau.

### 4.4.2. Wizara yenye Dhamana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

(a) Kutekeleza na kusimamia kwa karibu shughuli zote za Mwongozo zinazotekelezwa na Wadau mbalimbali katika ngazi za Mikoa na Halmashauri zote nchini;

(b) Kusaidia upatikanaji wa taarifa na takwimu husika za utekelezaji wa shughuli za Mwongozo;

(c) Kuhakikisha kuwa Mamlaka za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zinatenga bajeti kwa ajili ya utoaji wa huduma kwa Watu wenye Ulemavu;

(d) Kuimarisha ulinzi na usalama kwa Watu wenye Ulemavu kwa kushirikiana na Wadau na Jamii kwa ujumla; na

(e) Kuwasilisha taarifa kila robo mwaka ya utekelezaji kwenye Wizara yenye dhamana na masuala ya Watu wenye Ulemavu.

### 4.4.3. Mamlaka za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

(a) Kutekeleza Mwongozo huu kwa kuhakikisha utoaji wa huduma kwa Watu wenye Ulemavu unazingatia mahitaji ya msingi ili kujenga jamii jumuishi;

(b) Kutekeleza na kusimamia kwa karibu shughuli za kufanya utambuzi na kujua mahitaji ya Watu wenye Ulemavu katika jamii;

(c) Kutenga bajeti kwa ajili ya utoaji wa huduma bora na jumuishi kwa Watu wenye Ulemavu;

(d) Kushirikiana na Wadau na Jamii kwa ujumla ili kuimarisha ulinzi na usalama kwa Watu wenye Ulemavu;

(e) Kutoa matunzo kwa Watu wenye Ulemavu, pale inapostahiki, kwa kuwapa mahitaji muhimu ya maisha kulingana na hali zao;

(f) Kuandaa na kutekeleza mfumo wa kuwashirikisha Watu wenye Ulemavu kwenye vikao muhimu vya mashauriano na maamuzi katika ngazi ya Mkoa, Wilaya, Halmashauri, Kata, Vijiji na Mitaa hadi Vitongoji;

(g) Kuwajumuisha Watu wenye Ulemavu katika mipango ya uzalishaji mali na utekelezaji wake;

(h) Kufanya utambuzi wa Taasisi Binafsi zinazotoa huduma kwa Watu wenye Ulemavu na kufuatilia, kusimamia na kushiriki tathmini za utekelezaji wa shughuli za Taasisi hizo; na

(i) Kuunda na kuhakikisha kamati za watu Wenye Ulemavu zinatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria.

### 4.4.4. Wizara yenye Dhamana na Masuala ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

(a) Kutekeleza masuala yote ya kisera na kisheria kuhusu elimu, mafunzo na ujuzi kwa Watu wenye Ulemavu;

(b) Kuhakikisha upatikanaji wa huduma na mahitaji muhimu, ikiwemo wataalamu, nyenzo, vitendea kazi na vifaa saidizi kulingana na mahitaji na mazingira husika ya utekelezaji wa Mwongozo katika eneo la elimu na mafunzo; na

(c) Kuwasilisha taarifa za utekelezaji kwenye Wizara yenye dhamana na masuala ya Watu wenye Ulemavu kila mwaka;

### 4.4.5. Wizara zenye Dhamana na Masuala ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum

(a) Kutekeleza masuala yote ya kisera, usimamizi na kiuratibu kuhusu huduma za Afya, Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii kwa Watu wenye Ulemavu kama inavyoelekezwa na Mwongozo huu;

(b) Kuhakikisha ufikivu wa huduma za afya na ustawi wa jamii kwa Walengwa kwa viwango bora na wakati muafaka; na

(c) Kuwasilisha taarifa za utekelezaji kwenye Wizara yenye dhamana na masuala ya Watu wenye Ulemavu kila mwaka.

### 4.4.6. Wizara zenye Dhamana na Masuala ya Habari, Mawasiliano, Utamaduni, Sanaa na Michezo

(a) Kutekeleza masuala yote ya kisera, usimamizi na kiuratibu kuhusu huduma Katika maeneo husika kama inavyoelekezwa na Mwongozo huu;

(b) Kuweka mazingira wezeshi na fikivu kwa Watu wenye Ulemavu kuweza kujumuika katika huduma husika; na

(c) Kuwasilisha taarifa za utekelezaji kwenye Wizara yenye dhamana na masuala ya Watu wenye Ulemavu kila mwaka.

### 4.4.7. Wizara yenye Dhamana na Masuala ya Ujenzi, Miundombinu na Uchukuzi

(a) Kutekeleza masuala yote ya kisera, usimamizi na kiuratibu kuhusu huduma katika maeneo husika kama inavyoelekezwa na Mwongozo huu;

(b) Kuweka mazingira wezeshi na fikivu kwa Watu wenye Ulemavu kuweza kujumuika katika huduma mbalimbali za umma na jamii; na

(c) Kuwasilisha taarifa za utekelezaji kwenye Wizara yenye dhamana na masuala ya Watu wenye Ulemavu kila mwaka.

### 4.4.8. Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali na Taasisi nyingine za Serikali

Wizara, Idara, Mashirika na Taasisi nyingine za Serikali zina wajibu wa kuhakikisha kuwa: -

(a) Masuala ya Watu wenye Ulemavu yanahuishwa, kujumuishwa na kutekelezwa ipasavyo kwa Sekta husika, kulingana na mwelekeo wa Mwongozo;

(b) Mahitaji, ushiriki na ushirikishwaji wa Watu wenye Ulemavu yanazingatiwa ipasavyo katika utekelezaji wa Mwongozo na shughuli zao za kisekta na kitaasisi;

(c) Kusimamia na kutoa taarifa kwa wakati na gharama za mipango na utekelezaji wa bajeti kwa kutumia mipango mikakati, shabaha pamoja na hatua zilizochukuliwa kwa mujibu wa majukumu yao; na

(d) Kuwasilisha taarifa za utekelezaji kwenye Wizara yenye dhamana na masuala ya Watu wenye Ulemavu kila mwaka.

### 4.4.9. Sekta Binafsi na Wadau Wengine Muhimu

Utekelezaji wa Mwongozo huu utahusisha Asasi za Kiraia, Mashirika ya Kimataifa, Taasisi za Kidini, Asasi zisizo za Kiserikali pamoja na wadau wengine muhimu wanaojishughulisha na utoaji wa huduma kwa Watu wenye Ulemavu. Wajibu wao ni kama ifuatavyo: -

(a) Kuandaa na kuwasilisha taarifa ya hali ya utekelezaji wa mipango yao inayohusiana na eneo la Watu wenye Ulemavu kwa Wizara yenye dhamana na masuala ya Watu wenye Ulemavu kwa ajili ya kujumuishwa katika taarifa kuu ya utekelezaji;

(b) Kutekeleza Mwongozo huu kwa kuhakikisha utoaji wa huduma kwa Watu wenye Ulemavu unazingatia mahitaji ya msingi ili kujenga jamii jumuishi;

(c) Kutekeleza Mwongozo huu kwa kushirikiana na Serikali kuu, Mamlaka za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na wadau wengine katika kutekeleza Afua stahiki kwa Watu wenye Ulemavu;

(d) Kuendelea kuielimisha jamii kuhusu dhana ya ulemavu na maadili mema katika ujumuishwaji na uimarishaji wa huduma kwa Watu wenye Ulemavu; na

(e) Kuendesha shughuli zao kwa kuzingatia Maadili na Vipaumbele vya Mwongozo huu, hususan katika kusaidia upatikanaji wa rasilimali fedha, huduma na vifaa kwa ajili ya Watu wenye Ulemavu.

### 4.4.10. Shirikisho na Vyama vya Watu wenye Ulemavu

Wajibu wa Shirikisho na Vyama vya Watu wenye Ulemavu katika utekelezaji wa Mwongozo huu ni pamoja na: -

(a) Kuhakikisha utekelezaji wa majukumu yao unazingatia Vipaumbele vilivyoainishwa katika Mwongozo;

(b) Kuelekeza nguvu zao katika maeneo ambayo bado hayajafikiwa ili kuhakikisha utoaji wa huduma unazingatia haki, usalama, fursa sawa na ustawi wa Watu wenye Ulemavu;

(c) Kushirikiana na Wadau wengine ili kufanya utambuzi kwa lengo la kujua mahitaji ya Watu wenye Ulemavu;

(d) Kushirikiana na Mamlaka za Serikali Kuu na Serikali za Mitaa katika kutoa misaada ya kuboresha maisha kwa Watu wenye Ulemavu;

(e) Kuhamasisha na kuhakikisha ushiriki wa Watu wenye Ulemavu katika mipango na utekelezaji wa shughuli za uzalishaji mali; na

(f) Kuwasilisha taarifa za utekelezaji kwenye Wizara yenye dhamana na masuala ya Watu wenye Ulemavu kila mwaka.

#### 4.4.11. Watu wenye Ulemavu

(a) Kuhakikisha kuwa wanazifikia na kuzitumia fursa mbalimbali zilizopo katika maeneo yao; na

(b) Kuhakikisha wanatimiza ipasavyo wajibu wao katika jamii kwa kuzingatia maadili ya utekelezaji wa Mwongozo kwa misingi ya Vipaumbele vilivyowekwa.

## 4.5. Uratibu na Utekelezaji wa Mwongozo

Uratibu na utekelezaji wa Mwongozo huu utakuwa katika ngazi kuu mbili ambazo ni Mamlaka za Serikali; na Sekta binafsi na Washirika wa Maendeleo.

### 4.5.1. Mamlaka za Serikali

Uratibu wa utekelezaji wa Mwongozo huu utafanyika kwa kusimamiwa na Ofisi yenye dhamana na masuala ya Watu wenye Ulemavu. Aidha, Ofisi yenye dhamana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itaratibu utekelezaji wa Mwongozo katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ofisi itawajibika kufuatilia utekelezaji wa hatua mahsusi, kuandaa na kuwasilisha taarifa kwenye Wizara yenye dhamana na masuala ya Watu wenye Ulemavu.

Wizara yenye dhamana na masuala ya Watu wenye Ulemavu itapokea na kuchambua taarifa za utekelezaji wa hatua mahsusi zinazochukuliwa kutoka Wizara za Kisekta,

zikiwemo taasisi na Mashirika ainishwa na kuandaa taarifa ya tathmini ya utekelezaji wa Mwongozo kwa kila kipindi stahiki. Wizara itatoa taarifa rasmi ya utekelezaji wa Mwongozo kila mwaka.

### 4.5.2. Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia

Utekelezaji wa Mwongozo katika Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia utaratibiwa na Wizara yenye dhamana na masuala ya Watu wenye Ulemavu kwa kushirikiana na Wizara na Mamlaka za Kisekta. Kupitia na/au kwa kushauriana na Mamlaka za Kisekta; Wizara yenye dhamana na masuala ya Watu wenye Ulemavu itawajibika kufuatilia utekelezaji wa hatua mahususi zinazochukuliwa na Wadau husika katika uimarishaji huduma na kukuza ujumuishwaji wa Watu wenye Ulemavu kwenye mipango, bajeti na shughuli za Sekta husika.

# SURA YA TANO

## 5.0. UFUATILIAJI, TATHMINI, MAPITIO NA MAREKEBISHO YA MWONGOZO

### 5.1. Ufuatiliaji na Tathmini

Kila Mdau atapaswa kuwa na Mfumo Thabiti wa Ufuatiliaji na Tathmini ambao unajumuisha viashiria muhimu vya utekelezaji na namna ya kufanya upimaji stahiki wa utekelezaji wa maeneo makuu saba ya vipaumbele vya mwongozo huu. Njia za kuhakiki na kuthibitisha utekelezaji zioneshwe ili kurahisisha ufuatiliaji na tathmini.

Ufuatiliaji, utoaji taarifa na tathmini utazingatia utekelezaji wa kila jukumu lililoainishwa katika ngazi husika ya utekelezaji wa Mwongozo huu. Ufuatiliaji na tathmini kwa Wadau utafanikisha upatikanaji wa taarifa za utekelezaji na kufahamu kiwango cha mafanikio ya Sekta na Mdau husika katika utekelezaji wa vipaumbele vilivyowekwa.

Mafanikio ya utekelezaji wa mwongozo huu kwa kila Mdau yataonekana kwa kuzingatia mfumo wa ufuatiliaji na tathmini utakaoandaliwa na wizara yenye dhamana na watu Wenye Ulemavu. Kila eneo lililotajwa ndani ya Mwongozo huu, pamoja na vipaumbele elekezi kwa majukumu na shughuli zote vilivyoainishwa ni lazima ziwekewe mfumo thabiti wa ufuatiliaji wa kila siku kwa kila Mdau na hatimaye kuweza kufanyiwa tathmini ili kuona uelekeo na kupata picha halisi kwa kuzingatia malengo na shabaha walizo jiwekea kwa kuzingatia Mwongozo. Wadau wanapaswa kuandaa taarifa za utekelezaji wa Mwongozo huu na kuziwasilisha kwa mamlaka zao za usimamizi au mamlaka husika zilizoelezwa humu, kwa kila robo mwaka.

## 5.2. Mapitio na Marekebisho ya Mwongozo

Mapitio na Marekebisho ya Mwongozo yanaweza kufanyika kwa mapendekezo ya Wadau pindi itakapoonekana ni muhimu na ipo haja ya kufanya hivyo, kwa jambo lolote litakalobainika kwa kuzingatia mazingira pamoja na mahitaji halisi ya jamii kwa wakati husika baada ya kufanyika kwa tathmini za utekelezaji wake.

Filename: MWONGOZO WA UTEKELEZAJI NEW UJUMUISHWAJINA UMARISHAJI WA HUDUMA KWA WWU edited chapa FINAL 18 October 2022.docx
Directory: /Users/gpdodoma/Library/Containers/com.microsoft.Word/Data/Documents
Template: /Users/gpdodoma/Library/Group Containers/UBF8T346G9.Office/User Content.localized/Templates.localized/Normal.dotm
Title:
Subject:
Author: mugendi
Keywords:
Comments:
Creation Date: 22/11/2022 12:11:00
Change Number: 2
Last Saved On: 22/11/2022 12:11:00
Last Saved By: Microsoft Office User
Total Editing Time: 0 Minutes
Last Printed On: 22/11/2022 12:11:00
As of Last Complete Printing
Number of Pages: 67
Number of Words: 12,532 (approx.)
Number of Characters: 71,438 (approx.)